# NAFASI NA UTAMBULISHO WA MWANAMKE KATIKA *NATALA* NA *KIFO KISIMANI*

**NA: KETER EBRAHIM KIPYEGON**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**OCTOBA 2013**

## UNGAMO

“Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuio kingine chochote”

Keter Ebrahim Kipyegon

(Mtahiniwa)

Sahihi ------------------------------------------ Tarehe -----------------------------------

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu.

Dkt. Amiri Swaleh

Sahihi ______________________________ Tarehe ________________________

Prof. Kineene wa Mutiso

Sahihi ______________________________ Tarehe ________________________

# YALIYOMO


UNGAMO ........................................................................................................ i

YALIYOMO .................................................................................................... ii

KUTABARUKU ............................................................................................... v

SHUKRANI .................................................................................................... vi

MUHTASARI ................................................................................................. viii

ORODHA YA VIFUPISHO ............................................................................... x

**SURA YA KWANZA ........................................................................................ 1**

1.0 UTANGULIZI ............................................................................................... 1

1. Tatizo la utafiti. ........................................................................................ 2

1.2 Madhumuni Ya Utafiti. .............................................................................. 4

1.4 Sababu Za Kuchagua Mada ......................................................................... 4

1.5 Upeo na Mipaka ......................................................................................... 6

1.6 Misingi ya Nadharia ................................................................................... 7

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..................................................................... 13

1.8 Njia za Utafiti ........................................................................................... 16

**SURA YA PILI .............................................................................................. 17**

**NAFASI NA UTAMBULISHO WA MWANAMKE KATIKA *NATALA* ................ 17**

2.0 Utangulizi .................................................................................................. 17

2.1 Nafasi dhalilishi na duni ya mwanamke ...................................................... 18

2.1.1 Mwanamke Kama chombo cha kumfurahisha mwanamume. ...................... 19

2.1.2 Mwanamke kama kiumbe duni asiyeweza kumiliki chochote. ..................... 22

2.1.3 Mwanamke kama mtegemezi wa mwanamume ............................................. 26

2.1.4 Mwanamke kama mtu mwovu ..................................................................... 26

2.1.5 Mwanamke Kama mgomvi na mtu asiye na shukrani.................................... 27

2.1.6 Mwanamke Kama mbeya. ............................................................................. 27

2.1.7 Mwanamke kama msaliti anayetosheka na hali yake ................................. 28

2.2 Nafasi chanya anayopewa mwanamke katika jamii............................................ 29

2.2.1 Mwanamke kama mtu Jasiri ....................................................................... 30

2.2.2 Mwanamke anahitaji na anastahili kuwa uhuru wa kimawazo. ....................... 36

2.2.3 Mwanamke kama mlezi mwema wa watoto................................................... 37

2.2.4 Mwanamke kama mtu mkakamavu. ............................................................... 39

2.2.5 Mwanamke kama mtu mwerevu. ................................................................... 40

2.3 Hitimisho ........................................................................................................... 41

**SURA YA TATU ............................................................................................... 42**

3.0 Utangulizi ........................................................................................................... 42

3.1 Nafasi Dhalilishi na dunishi anayopewa mwanamke............................................ 42

3.1.1 Mwanamke kama chombo cha kumfurahisha mwanamume........................... 43

3.1.2 Mwanamke kama mmbeya ............................................................................ 44

3.1.3 Mwanamke kama barakala. ............................................................................ 46

3.1.4 Mwanamke kama kiumbe duni asiyestahili heshima. ..................................... 47

3.1.5. Mwanamke kama mtu mwenye hasira za mkizi............................................ 50

3.1.6 Mwanamke kama mtu anayedanganyika kwa haraka .................................... 51

3.2 Nafasi chanya na ya kimapinduzi anayopewa mwanamke .................................... 51

3.2.1 Mwanamke kama mtu mwenye bidii............................................................. 52

3.2.2 Mwanamke kama mtu mwenye mapenzi ya dhati ........................................ 55

3.2.3 Mwanamke kama mtu mwerevu na mwenye akili tambuzi. ............................ 57

3.2.4 Mwanawake kama mzalendo jasiri ................................................................ 61

3.3 Hitimisho ............................................................................................................ 65

**SURA YA NNE ........................................................................................................ 67**

4.0 Utangulizi ............................................................................................................ 67

4.1 Asasi za Kitamaduni ............................................................................................ 67

4.1.1 Asasi ya Ndoa ...................................................................................................... 70

4.1.3 Uhafidhina ............................................................................................................ 72

4.1.4 Wanawake kutoshirikishwa katika maamuzi .................................................... 75

4.2 Hali ya kutojua miongoni mwa wanawake wenyewe. ........................................ 77

4.3 Mfumo wa Kichumi ............................................................................................ 79

4.4 Ukosefu wa Ushirikiano Miongoni mwa Wanawake Wenyewe. ......................... 81

Hitimisho ................................................................................................................... 83

**SURA YA TANO ...................................................................................................... 85**

HITIMISHO ............................................................................................................... 85

5.0 Utangulizi ............................................................................................................ 85

5.1 Muhtasari wa Matokeo ya utafiti. ........................................................................ 85

MAREJELEO ............................................................................................................ 91

## KUTABARUKU

Naitaburuku kazi hii kwa wazazi wangu: Elizabeth Kirui na Kipketer Kirui (Konyif), kwa maazimio mema waliyokuwa nayo. Pia mke wangu Judy Keter na watoto Faith Chelangat na Emmanuel Kiprotich. Sitawasahau walimu wangu wote wa Kiswahili na hasa Bw. Philip Mutai. Hatimaye, Mhubiri Paul Rotich, wa Mogoiwet ‘African Gospel Church’.

## SHUKRANI

Tasnifu hii haingeweza kukamilika bila ya usaidizi, uongozi na mchango wa watu wengi. Ni vigumu kuwataja wote, nitawataja wachache tu.

Ningependa kutoa shukrani maalum kwa wahadhiri na wasimamizi wangu Dktr. Amiri Swaleh, na Prof. Kineene wa Mutiso kwa mawaidha na ushauri wao. Walinisahihisha na kuniongoza pale nilipokosea katika utafiti na masuala yanayohusu utafiti. Ninawashukuru kwa kuwa wavumilivu na wapole kunishauri hata pale nilipoteleza. Ni kwa umakinivu na kunielewa ndipo nikafanikisha kazi yenyewe kiwakati. Mawaidha yao mema yalinitia hari na mshawasha wa kumakinikia kazi yenyewe na kuandika kazi bora. Mola awe nanyi, ampe hekima na Baraka zake.

Shukrani za dhati pia nazitoa kwa wahadhiri wengine katika idara ya Isimu na Lugha ya Chuo Kikuu cha Nairobi walionisaidia na kunielekeza katika kazi hii ya usomi. Hawa ni: Dktr. Evans Mbuthia, Dktr. Zaja Omboga, Dktr. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Bw. B.G. Mungania na Dktr. Jefwa Mweri, sitasahau wakufunzi wenzangu tulioshirikiana nao katika safari hii ya kutafuta shahada ya uzamili. Namshukuru nyote, na hasa mwakilishi wa darasa Bw. Wilson Chacha Caleb, mchango wenu umekuwa johari kwangu. Bi. Lily Chebet, Bw. Joseph Makange na Bw. Justus Ndumbu, sitasahau msaada wentu wa kipekee mlionipa wakati huo.

Kwa mke wangu mpendwa Bi. Judy Keter, shukrani nyingi na Baraka za Maulana kwako. Usaidizi wako na kunielewa kulinifanya nianze, niendelee na kuhitimisha safari

hii. Kwa wanangu Faith Chelangat na Emmanuel Kiprotich, nasema ahsante kwa uvumilivu wenu mwingi. Sitawasahau dadangu Bi. Hellen Kikwai, Purity Chepkemoi, Maurin Cherono na waumini wote wa kanisa la 'African Gospel Church' Mogoiwet na Kiptergekian- kwa kusabilia kuwa nami katika maombi na motisha kila wakati.

Nasheheneshа pia shukrani zangu za dhati kwa Bw. Collins Ngetich, Bw. Geoffrey Rono, Bw. Raphael Koech, Bi. Emily Bett, Bw. Francis Chebole, Bw.David Rotich, Bw. Julius Bett, Bw.Weldon Bett, Bw. Richard Langat, Bw. Raphael Yegon, Bi. Janeth Mutai, Bi. Vicky Maritim Bi. Anne Langat, Bw.Joseah Cheruiyot, Bw. Wesley Rono, Bw. Emmanuel Bunei, Bw. Stanley Langat na Bw. Barnabas Koech- wa shule ya Upili ya Solyot. Shukrani na Mungu ambariki nyote.

Hatimaye, ninawashukuru wafuatao kwa msaada wao katika shughuli zote za upigaji chapa; Bi. Wilfrida Koskey, Bw. Ken Kosgey, Bi. Sylvia Akendo wa Chuo Kikuu Cha Nairobi. Mbarikiwe sana kwa msaada wenu usio na kifaani.

# MUHTASARI

Madhumuni katika utafiti wetu yalikuwa ni; kwanza kuchunguza taswira chanya ambazo mwandishi anaangazia kumhusu mwanamke katika Natala na Kifo Kisimani. Pia, tulichunguza changamoto zinazokabili mwanamke katika harakati zake za kujikomboa.

Katika kufikia madhumuni yenyewe, tulihitajika kusoma kwa mapana, kuhakiki na kuvichambua vitabu vinavyohusu nafasi ya mwanamke. Pia, tulihitajika kusoma vitabu vinavyoangazia nadharia ya Ufeministi.

Katika utafiti wenyewe, tuliongozwa na nadharia ya Ufeminsiti wa Kiafrika. Kwa ujumla, nadharia ya Ufeministi ni nadharia yenye malengo maalum. Hulenga kuangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii ya ki-ubabe-dume.

Kutokana na utafiti wetu, ilibainika kuwa Kithaka wa Mberia amefaulu vilivyo kumsawiri mwanamke katika jamii ya ki-ubabedume. Anaonyesha nafasi chukivu anayopewa mwanamke katika jamii ya aina hii. Licha ya hayo, mwandishi anatoa mchango wake muhimu katika kumjenga mwanamke kihadhi.

Tasnifu yenyewe ina sura tano: sura ya kwanza inaangazia somo la utafiti, sura yenyewe lina utangulizi, tatizo la utafiti, madhumuni, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mpaka ya utafiti, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti.

Sura ya pili inaangazia nafasi na utambulisho wa mwanamke kama unavyodhihirika katika *Natala* (1997). Sura yenyewe inadokeza nafasi dhalilishi na dunishi katika sehemu ya kwanza, na nafasi chanya katika sehemu ya pili. Sehemu ya tatu ni hitimisho.

Sura ya tatu inahusu nafasi na utambulisho wa mwanamke kama unavyojitokeza katika *Kifo Kisimani* (2001). Sehemu ya kwanza inaangazia nafasi dhalilishi na dunishi. Sehemu ya pili ni nafasi chanya, sehemu ya tatu ni hitimisho.

Sura ya nne inaangazia changamoto zinazokabili harakati za kumkomboa mwanamke. Changamoto zenyewe ni za aina aina, kama yanavyodhihirika katika tamthilia hizi.

Sura ya tano ina hitimisho ya tasnifu yenyewe. Katika sura yenyewe, kuna ithibati kubainisha kutimia kwa madhumuni ya utafiti wenyewe.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| Bi | - | Bibi |
| Bw | - | Bwana |
| Dktr | - | Daktari |
| Prof. | - | Profesa |
| Khj | - | Kama hapo juu |
| Uk | - | Ukurasa |
| Mh. | - | Mhariri |
| TY | - | Tafsiri yetu |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Katika utafiti huu, tunanuia kuchunguza nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala* (1997) na *Kifo Kisimani* (2001). Katika utafiti wenyewe, maana ya istilahi 'nafasi' ni umuhimu au heshima inayopewa kitu au mtu. Nayo istilahi utambulisho inatumiwa kama anavyoieleza Cabral (1975:64) kuwa sifa na matumaini ya pamoja yanayombainisha mtu au kikundi cha watu wenye sifa sawa zinazowatambulisha za kihistoria, kibiolojia au kijamii katika kipindi maalum cha maendeleo yao.

Utafitiwetu utaangazia jinsi ambavyo mwandishi mwanamume amefaulu katika usawiri wake wa mwanamke kwa kutambulisha nafasi yake bayana katika jamii. Tunamchunguza mwandishi Kithaka wa Mberia kwa kurejelea tamthilia za *Natala* na *Kifo Kisimani.*

Wasanii mbalimbali wameshiriki vita hivi katika harakati hizi za kumkomboa mwanamke. Kulingana na Mukobwa (1985), wasanii hudhihirisha vipawa vyao kwa namna tofautitofauti. Miongoni mwao ni yule ambaye licha ya kudhihirisha matatizo yanayowakabili wanajamii, ana imani kwamba yanaweza kutatuliwa. Kazi ya mwandishi kama huyu inatoa suluhu ya kufikia hali iliyo shwari. Kulingana na Mukobwa, mwandishi Kama huyu huchochea wanajamii watatue matatizo yanayowakabili kwa kutafakaria suluhisho yake. Anaendelea kueleza kwamba mwandishi kama huyu ni wa kimapinduzi.Huwa na ndoto ya kuwa na jamii mpya inayowahimiza watu katika harakati za kujikomboa na kujiendeleza.

Kumekuwepo na dhana kuwa vita vya ukombozi wa mwanamke kutokana na ubabe-dume ni vita vinavyowahusu wanawake pekee. Hivyo basi, mwandishi mwanamke huchukuliwa kuwa mtetezi wa haki za mwanamke mwenzake. Kwa maoni yetu, vita vya ukombozi wa mwanamke ni vita vya kijamii na hivyo basi wanaume kwa wanawake wanapaswa kushiriki kwa njia moja au nyingine. Na kama anavyosema Mugambi (1982) kwamba, fasihi ni silaha mojawapo katika ghala ya silaha nyingi zinazotumiwa na tabaka (kundi) moja kutetea maslahi yake katika mapambano, tungependa tuthibitishe ukweli huu kwa kuangazia tamthilia mbili za Kithaka wa Mberia.

Utafiti wetu unanuia kuchunguza namna mwandishi mwanamume anavyotumia silaha hii katika mapambano hayo. Pia, tutazingatia mchango wa mwandishi mwanamume katika kuwaunga mkono wanajamii wenzake (wanawake) katika vita hivi. Tumechukulia kuwa hivi ni vita vya kijamii hasa nyakati hizi ambapo pana harakati za ujenzi wa jamii mpya.

Utafiti wetu utajikita katika tamthilia mbili za Kithaka wa Mberia kwa kutambua namna mwandishi anavyoendeleza nafasi ya mwanamke katika kazi zake. Kazi zenyewe ni *Natala* (1997) na *Kifo Kisimani* (2001).

## 1. Tatizo la utafiti.

Mapambano ya kupigania haki na usawa miongoni mwa wanaume na wanawake yameendelea kwa muda mrefu. Haya ni tangu kuasisiwa kwa vuguvugu la Ufeministi linalohoji taswira dhaifu na dunishi ya mwanamke katika jamii. Ingawa harakati za

vuguvugu lenyewe kwa kiwango fulani zimezalisha matunda, bado pana haja ya kuimarishwa zaidi.

Hayo yanatokana na dhana kuwa harakati zenyewe ni za jinsia moja yaani za mwanamke kwa sababu ndiye anayeathirika moja kwa moja. Waandishi wanawake wamejaribu kutumia kazi za sanaa kubadili mtazamo huo. Dhana kuwa ni harakati za mwanamke kujitetea kwa sababu ni mwathiriwa pekee kwa maoni yetu, si kweli kwani hata waandishi wanaume nao wanaangazia suala lenyewe.

Anavyosema Mugambi (1982) ni kweli kwamba fasihi ni silaha mojawapo katika ghala ya silaha nyingi zinazotumiwa na tabaka moja (na wahisani wao) kutetea maslahi yake katika mapambano. Kwa hivyo, vita vya kumkomboa mwanamke vimewashirikisha waandishi ambao wanajaribu kujenga taswira chanya ya mwanamke na wakati huo huo kuangazia vizingiti vinavyokwaza ufanisi huu wa ukombozi wake.

Katika utafiti huu, tunanuia kuchunguza ni vipi ambavyo Kithaka Wa Mberia ameweza kufanikisha usawiri wa mwanamke na kubainisha nafasi yake kama ilivyo katika jamii ,inayodhibitiwa na mfumo wa ubabe-dume. Twajiuliza: Je, amejenga hadhi ya mwanamke? Na je, ameangazia vipi vizingiti vinavyokwamiza ufanisi wa ukombozi wa mwanamke?

Kulingana na maoni yetu, hakuna kazi nyingine ambayo imefanywa katika kushughulikia mada hii kwa kurejelea kazi hizi mbili za mwandishi huyu. Hilo ndilo pengo ambalo tunanuia kuliziba.

## 1.2 Madhumuni Ya Utafiti.

I. Kuchunguza taswira chanya ambazo mwandishi anaangazia kumhusu mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani*.

II. Kubainisha changamoto zinazomkabili mwanamke katika harakati zake za kujikomboa, kwa kurejelea kazi za mwandishi huyu mwanamume.

## 1.3 Nadharia Tete.

(I) Katika tamthilia ya *Natala* na *Kifo Kisimani*, mwandishi amefaulu kubainisha nafasi ya mwanamke kama ilivyo katika jamii.

(II) Mwandishi amefaulu kumtafakarisha mwanamke kuchukua hatua za kuzikabili changamoto zinazomkabili katika jamii.

## 1.4 Sababu Za Kuchagua Mada

Uteuzi wa mada hii umetokana na sababu zifuatazo:

Kwa kuamini kuwa Kithaka wa Mberia ni miongoni mwa waandishi wanaume wanaotambulika katika kuwajenga wanawake kihadhi na kutambua uwezo wao. Huyu ni msanii ambaye punde alipoingia katika uwanja wa utunzi, kwa maoni yetu, alijiingiza katika harakati za kupigania usawa wa kijinsia. Amekuwa, kwa maoni yetu, katika mstari wa mbele kuihamasisha jamii kuhusu utangamano bora wa kijinsia ilhali mchango huu

wake kwa kiasi fulani haujaangaziwa na wahakiki kwa pakubwa. Kuna wale waliomhakiki lakini tumeamua kuhakiki kazi zenyewe kwa undani ili kutambua mchango wake kuhusu suala hili.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii imetokana na maoni yetu kwamba, kwa kiasi fulani, kumekuwepo na dhana kuwa vita vya kumkomboa mwanamke ni vya mwanamke pekee. Kwamba, mchango wa mwandishi mwanamume haujatambuliwa pakubwa katika harakati hizi. Tunaamini kuwa mwandishi ni mwanajamii mwenye ndoto ya kuiboresha jamii na hivyo, kuangazia nguvu na udhaifu wa jamii kwani fasihi ni kioo cha jamii.
Kuna waandishi wanaume ambao nao wamemsawiri mwanamke kwa kumpa nafasi chanya. Tungependelea kuziangazia kazi hizo lakini kwa ajili ya kuchunguza kwa undani na ubora, haingewezekana. Tumemteua Kithaka wa Mberia kwa sababu kwa maoni yetu, amesana kazi zake kwa namna ambavyo inadhihirisha uelewa na utambuzi wake wa hali halisi katika jamii. Hivyo basi, anaangazia hali yenyewe na kumpa msemaji kutafakaria na hivyo kutafuta suluhu kwayo.

Sababu nyingine ni kwamba, ni muhimu suala hili lishughulikiwe hasa wakati huu ambapo jamii inapitia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika nchi mbalimbali Kenya ikiwemo, suala la wanawake na uongozi huipiga mshipa kila jamii. Hii ina maana mwanamke sharti atambuliwe na apewe haki yake katika jamii hasa katika ngazi za uongozi. Hii ina maana kuwa mwanamke pia anaweza kuongoza. Hii ndiyo sababu nyingine iliyotushawishi kujikita katika uchunguzi wetu. Tunajiuliza je, wanaume wanatambua uwezo huo wa wanawake? Maoni yetu ni kwamba, mwandishi

ana mchango wa kudhihirisha uwezo wenyewe kupitia kazi zake za kifasihi kwa kumsawiri mwanamke kwa namna fulani. Kwa hivyo, swali tunalojiuliza ni je, Kithaka wa Mberia amewasawiri vipi wahusika wake wa kike?

Twatumai kuwa mchango huu wetu utaongeza uhamasishaji wa waandishi wanaume ili wawe kiunzi muhimu katika kuleta ufanisi katika harakati za kumkomboa mwanamke na vilevile kumjenga kihadhi katika jamii za ki-ubabedume .

## 1.5 Upeo Na Mipaka

Utafiti wetu ni wa kifasihi na hivyo basi tunanuia kujishugshulisha na uhakiki wa tamthilia mbili zilizoandikwa na Kithaka wa Mberia kwa kuangazia nafasi ya mwanamke katika kazi zenyewe. Kazi zenyewe ni; *Natala* (1997) na *Kifo Kisimani* (2001).

Katika uhakiki wetu, tunalenga kutathmini mchango wa mwandishi huyu katika kumwangazia mwanamke kwa kumwinua kihadhi ili kufichua changamoto zinazomkabili katika harakati za kujitambua na hivyo kupata “hadhi” mpya kijamii.

Tutajikita pakubwa katika tamthilia mbili. Hata hivyo ikibidi, tutapanua mawanda yetu kwa kurejelea na kudurusu kazi nyingine zitakazotusaidia kuendeleza utafiti wetu uwe bora zaidi.

## 1.6 Misingi ya Nadharia

Utafiti wetu utaongozwa na nadharia ya Ufeministi. Hii ni kwa sababu tunanuia kuangalia ni vipi mwandishi amefaulu kumsawiri mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani*. Nadharia hii iliasisiwa kwa lengo la kuangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Matatizo yenyewe yanasababishwa na tofauti za kijinsia. Kwa maoni ya waasisi wa nadharia hii, matatizo yanayomkabili mwanamke yamejengeka kwenye misingi ya jinsia yao. Hii ina maana kuwa mwanamke amewekwa katika hadhi au daraja fulani katika jamii.

Kulingana na Wamitila (2003:253), Ufeministi ni nadharia inayopinga asasi zote za kijamii zinazochangia katika kudhulumiwa kwa mwanamke. Wafuasi wa nadharia hii wanashikilia kwamba, pana haja ya kuwa na usawa wa kijinsia licha ya kuwapo kwa tofauti za kimaumbile. Kwa hivyo, wote wanaelekea kukubaliana kuwa, wanawake wanafaa wajitokeze kupigania haki zao ili angaa kuwe na usawa wa kijinsia.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007:92), kuna njia mbili za kubainisha matapo tofauti ya nadharia ya Ufeministi. Kuna uainishaji unaoangazia masuala ya wanawake kimaeneo na uainishaji unaozingatia mirengo ya kiitikadi. Tutaangalia aina zote mbili. Uainishaji wa kimaeneo, kulingana Wafula na Njogu, ulifanywa kwa kuzingatia changamoto zinazowakabili wanawake katika maeneo mbalimbali. Uainishaji huu ulitokana na ufahamu kwamba, wanawake wanakabiliwa na matatizo na changamoto tofautitofauti kutegemea maeneo wanakotoka. Waligawa sehemu zenyewe katika makundi manne: Ufaransa, Marekani, Uingereza na Afrika.

Kulingana na wahakiki hawa wa kifeministi, wanawake wa Ufaransa walitilia mkazo matumizi ya lugha. Kwamba lugha ilitumiwa kwa kumpendelea mwanamume. Wanawake wa Marekani waliwaunga mkono wale wa Ufaransa. Nao wakasema kuwa ni lugha na maandishi yaliyomtofautisha mwanamke na mwanamume. Wao walizingatia maandishi, namna mwanamke alivyojieleza na kukariri dhamira fulani katika maandishi yao.

Wanawake wa Uingereza nao walitilia mkazo suala la siasa na historia. Kwa maoni ya wanawake hawa wa Uingereza, wenzao wa Marekani walisisitiza zaidi masuala ya kihisia na sanaa, na kusahau historia na siasa. Wanawake wa Afrika nao wakawa na mtazamo tofauti na wenzao wa Ulaya na wale wa Marekani. Kwao, suala la utamaduni ndilo liliwakabili. Suala hili lilikuwa linawanyima nafasi ya kujieleza kwa namna mbalimbali; kuwakosesha nafasi ya kujieleza, uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi wa mwanajamii, tohara na ukeketaji pamoja na desturi zilizomdharau mwanamke asiyezaa. Kwetu, tutazingatia mwelekeo wa Kiafrika kwani tunaangazia masuala yanayowahusu wanawake wa bara la Afrika na hasa eneo la Afrika Mashariki.

Uainishaji wa pili kama wanavyoangazia Wafula na Njogu, ulifanywa na Adamson, Briskin na McPhail. Wahakiki hawa walizingatia mirengo ya kiitikadi. Mirengo yenyewe ilizua mirengo mitatu ambayo ni; ufeministi huru, ufeministi wa kiharakati na ufeministi wa kijamaa. Ufeministi huru hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Mkondo wenyewe hushikilia kwamba, maadamu wanadamu

wameumbwa kuwa viumbe sawa, wote wanawake kwa wanaume wanapaswa kuwa huru kutekeleza majukumu na malengo yao.

Ufeministi wa kiharakati humchukulia mwanamume kuwa adui mkubwa kabisa wa mwanamke. Waitifaki wake wanaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio ambao hutumiwa na mwanamume kumdhalilisha. Kwa maoni yao, suluhu ni kuwahimiza wanawake wasiolewe na wanaume. Badala yake wanawake wanahimizwa kushirikiana wao kwa wao hata kimapenzi.

Ufeministi wa kijamaa nao hulenga kukosoa ujamaa wa kimapokeo ambao licha ya kudai kwamba msingi wa unyonyaji ni jamii ya kitabaka inayompa mwanamume uwezo wa kumiliki njia kuu za kuzalisha mali, kutumia mali hiyo kadiri ya uwezo wake, huendeleza utabaka katika misingi ya kijinsia. Mrengo huu unawahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhia nyingine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za mwanamke. Utafiti huu wetu utaegemea Ufemenisti wa eneo la Kiafrika. Huu ni Ufemenisti unaozingatia suala la utamaduni. Ufeministi wa Kiafrika hasa ule unaohusisha fasihi unajishughulisha na hali halisi katika jamii za Kiafrika. Nadharia yenyewe inaangazia jinsi miktadha tofautitofauti inavyochangia katika unyanyasaji, udunishaji na udhalilishaji wa mwanamke wa Kiafrika. Wataalamu wanaounga mkono nadharia hii wanaeleza hali kinzani. Kwao, badala ya wanawake kuyakabili matatizo yaliyomo, wengi wao wanayakwepa. Wanadhihirisha mielekeo ya kutaka kufurahisha na kutojali hali yenyewe. Hatua hii inamtia motisha mwanamume kumgandamiza mwanamke na kujihifadhia hadhi yake ya juu.

Mwasisi wa Ufeministi huu wa Kiafrika ni Filomena Steady (1981) anayefanua matarajio ya nadharia yenyewe. Kwake, nadharia inafaa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazorutubisha unyanyasaji wa wanawake katika jamii. Nadharia yenyewe ina teneti zifuatazo:

- Inadhihirisha nia na malengo mahsusi yanayotokana na hali halisi katika jamii za Kiafrika.
- Inatambua historia ya jamii za Kiafrika, ambazo zilikuwa na watawala na mashujaa wanawake.
- Inachunguza hali ya mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya.

Hivyo basi, nadharia hii ya Ufeminsti wa Kiafrika ni nadharia itakayotufaa zaidi. Itatufaa katika utafiti wetu wa kuchunguza nafasi na utambulisho wa mwanamke. Kwa maoni yetu, ni nadharia mwafaka inayotetea haki na usawa wa kijinsia katika jamii.

Wafula na Njogu (2007:90) wanaelezea kuwa nadharia yenyewe inajumlisha mikabala mbalimbali ya kihakiki ambayo licha ya tofauti zake, inaelekea kukubaliana na kuafikiana kwenye masuala ya kimsingi. Kwanza, nadharia yenyewe imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa wanawake kutokana na pingu za kitamaduni, kidini, kisiasa na kiuchumi. Kwa maoni yao hizi ni pingu ambazo zimejengeka kwenye msimamo na itikadi ya kiume. Kudhulumiwa kwa mwanamke kumerutubishwa na mfumo wa ki-ubabedume unaomwenzi mwanamume na kumtweza mwanamke. Misingi hii ndiyo itakayotuongoza katika tathmini yetu.

Wollstonecraft (1792) ndiye anayetambuliwa kwa kuanzisha harakati za kumkomboa mwanamke kutokana na 'pingu' za kijamii zinazotokana na misingi ya ki-ubabedume na mpangilio wa kiume katika jamii. Katika kazi yenyewe, *A Vindication of the Rights of Women* (1792), mfeministi huyu aliupinga mfumo wa ki-babedume. Kwake mfumo wenyewe uliwapotosha vijana kiasi cha kuwafanya watambue 'uwezo' wa kiume katika jamii na kujitambulisha kwao au kulazimishiwa kuitikia desturi ya jamii yenyewe. Kama hatua ya kupiga vita mpangilio kama huo, Wollstonecraft alipendekeza elimu ya kibinafsi kwa nia ya kumtenganisha mtoto na ubabe-dume au wanafunzi wachanganywe madarasani na kupewa fursa ya kufurahia ujana wao na wakati huo huo wapewe shughuli za kutekeleza kwa ushirikiano. Anapinga vikali mazoea yaliyopelekea kutwezwa kwa mwanamke. Elimu ndicho chombo cha kupelekea usawa wa kijinsia na ukombozi wa mwanamke. Anafichua hali ambapo mwanamke hutazamwa kama mwanamke ndipo baadaye aonekane kama binadamu. Anasema mtazamo huu ndio unaomdunisha na kumpa mwanamke hadhi ya chini baada ya mwanamume.

Mapendekezo ya Mary Wollstonecraft ni kuundwa kwa jamii mpya yenye usawa kati ya mwanamke na mwanamume. Mawazo haya yanaungwa mkono na Simone de Beauvoir katika kazi yake ya *The Second Sex* (1949). Beauvoir anazishambulia asasi za kitamaduni zilizojengwa kwenye imani ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume kiasi cha kumchukulia mwanamke kama kiumbe duni. Alikuwa na mawazo sawa na ya Wollstonecraft kwamba, jamii inaendeleza taswira fulani chukulizi kumhusu mwanamke. Inamwangalia mwanamke kama kitu hasi ilhali mwanamume ni binadamu kielelezo. Kwa mujibu wa Wamitila (2002:157), Beauvoir anasisitiza kuwa utamaduni anamokulia

mwanamke huchangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo hivyo basi, unamfanya na hata kumlazimisha mwanamke kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni.

Millet (1969) naye katika kazi yake ya *Sexual Politics*, anashiriki vilivyo katika kutetea haki za wanawake kwa kupinga namna ambayo waandishi wanaume wanavyowasawiri wahusika wao wa kike. Anarejelea kazi za waandishi Henry Miller, Norman Mailer na Jean Genet.

Kulingana na Millet (1969:20), malezi ndiyo chanzo cha hali dhalilishi na duni ya mwanamke katika jamii. Kwa kuwa mtoto mvulana analelewa kwa namna ya kumdhihirishia sifa za uume: kujikidhia 'haja' za kiume. Malezi hayo yanamwandaa na kumtambulishia kuwa uume unahusisha matumizi ya nguvu, utundu na umilikaji wa kila kitu. Anaendelea kusema kwamba limekuwa jambo la kawaida ingawa si dhahiri katika jamii kwamba, mwanamume anamtawala mwanamke (1969:24). Torril Moi (1985) katika *Sexual/Textual Politics* anaelezea uwili unaojitokeza katika jamii. Anasema kuwa kila jinsia hunasibishwa na sifa fulani. Mwanamume hunasibishwa na jua kisitiari, na mwanamke hunasibishwa na mwezi.

Kazi hizi zitakuwa dira katika kazi yetu ya kiutafiti. Mawazo yao yatatuelekeza kutathmini namna ambavyo mwandishi amemsawiri mwanamke na vilevile changamoto zinazomkabili katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa kiume.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Masuala yanayowahusu wanawake ni muhimu na huibua hisia tofauti katika jamii hasa wakati huu ambapo wanawake wanaanza kujitambua na kushiriki kikamilifu katika ujenzi mpya wa jamii. Licha ya hayo, mwanamke ameanza kujitambua na wanaume nao wanatambua mchango muhimu wa wanawake katika jamii. Suala hili hivyo basi, limewapa wanajamii changamoto na kuwatia hamu ya kuchunguza na kuangazia masuala yanayouhusu usawa wa kijinsia. Tafiti nyingi zimefanywa katika kuliangazia suala lenyewe.

Udurusu wetu wa yaliyoandikwa umetutia moyo na wakati huo huo kutugusa kwani kuna kazi nyingi zilizotafitiwa kuhusu wanawake. Si riwaya si tamthiliia si ushairi, zote zimetafitiwa. Hata hivyo, tutaangazia machache yatakayokuwa na umuhimu zaidi kwetu.

Ndungo (1985) anatafitia maendeleo ya mwanamke na mabadiliko ya kihistoria katika fasihi ya Kiswahili. Anaangazia aina mbalimbali za ukandamizwaji zilizomkabili mwanamke katika mifumo tofauti ya kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Anasema kuwa mwanamke amefanywa kuwa chombo cha mwanamume cha kujifurahisha. Na kwamba mwanamke anaishi kulingana na matakwa ya mwanamume. Anaeleza namna ambavyo dini inatumiwa kumkandamiza na kumdhalilisha mwanamke. Akiangazia *Utenzi wa Mwanakupona*, anasaili namna asasi za kijamii zinavyomdhalilisha mwanamke. Anaangazia pia riwaya ya *Kaburi BiIa Msalaba.* Anasawiri nafasi muhimu na mchango aliotoa mwanamke katika harakati za kupigania ukombozi wa jamii licha ya changamoto nyingi zilizomkabili.

Totauti na kazi ya Ndungo, aliyeshughulikia tanzu mbili (ushairi na riwaya), tutaangazia nafasi n utambulisho wa mwanamke katika tamthilia mbili za Kithaka wa Mberia, *Natala* na *Kifo Kisimani*.

Kazi nyingine zitakazotufaa ni kama tasnifu ya Nyamberi (1997) aliyeangazia "Mwamko wa Mwanamke katika Tamthilia za Penina Muhando". Mhakiki huyu anaangazia namna mwanamke ameanza kutambua haja ya kupigania usawa wa kijinsia katika jamii yenye mfumo wa ki-babedume. Sawa na jinsi anavyoshughulikia kazi yake, kazi yetu itashughulikia taswira chanya ya mwanamke na pia mchango wa mwandishi katika kufichua changamoto katika ukombozi wenyewe. Tofauti ni kuwa Penina ni mwandishi wa kike ilhali tunahakiki kazi zake mwanamume. Pia, Nyamberi alitumia nadharia ya Ufemenisti asilia lakini tutatumia nadharia ya Ufemenisti wa Kiafrika. Lengo ni kutathmini changamoto zinazowakabili wanawake katika jamii za Kiafrika.

Maingi (2005) naye katika utafiti wake wa kuchunguza na kutathmini "Upembezwaji wa Mwanamke katika Udokezi wa Nafasi ya Mwanamke katika Utenzi wa Fatumah". Anaonyesha namna ambavyo mwanamke anapembezwa kwa kutoshirikishwa katika maamuzi muhimu ya kijamii ilhali anasifiwa kwa mchango wake wa kuwalea watoto nyumbani. Kazi hii itakuwa na umuhimu kwetu kwani itatuangazia zaidi asasi zinazomtweza mwanamke. Hata hivyo, tofauti ni kuwa mhakiki huyu aliangazia kazi ya ushairi ilhali sisi tutaangazia tamthilia. Katola (2006) katika uchunguzi wake wa kutathmini *Hatia*, *Buriani, Mama Ee,* na *Kitumbua Kimeingia Mchanga,* anaangazia namna ambavyo waandishi wanaume wameshiriki katika kuangazia udhalimu

unaoendelezwa katika jamii. Mhakiki huyu anaangazia udhalimu dhidi ya mwanamke katika jamii ilhali yetu tutaangazia nafasi na utambulisho wa mwanamke kwa ujumla kwa kurejelea kazi mbili za mwandishi mmoja wa kiume. Pia tutapiga hatua moja zaidi na kuangazia changamoto zinazomkabili mwanamke katika kufanikisha harakati za ukombozi. Sawa na utafiti wetu, mhakiki huyu anatumia nadharia ya Ufemenisti ya Kiafrika.

Mulila (2009) naye anatathmini usawiri wa mwanamke katika tamthilia za *Zilizala* na *Chamchela*. Anaeleza namna ambavyo waandishi wa tamthilia hizi (Njogu Kimani na Timothy Arege) wamechangia katika ukombozi wa mwanamke kwa kuonyesha taswira chanya na kumjenga mwanamke kihadhi. Kazi hii itatufaa sana kwani tunachunguza mchango wa mwandishi mwanamume sawa na mhakiki huyu. Tofauti ni kuwa tutaangazia kazi za mwandishi mmoja, Kithaka wa Mberia ilhali alichunguza waandishi wanaume wawili.

Mirikau (2011) katika utafiti wake, alichunguza taswira ya mwanamke katika tamithilia zake Wamitila. Anadhihirisha namna ambavyo mwanamke ana utegemezi mkubwa wa kiuchumi na hata kifikra ilhali bado analimbikizwa mzigo mzito katika jamii. Hii ni taswira mojawapo anayoangazia mhakiki huyu. Hata hivyo, anaonyesha namna ambavyo mwanamke mwenyewe amedhihirishwa kuwa anaweza kuongoza vyema akipewa nafasi. Hayo anayasema akiangazia taswira ya mwanamke katika *Pango*. Mhakiki huyu anaeleza namna ambavyo mwandishi amefaulu kumsawiri mwanamke katika kazi yake. Kazi hii itakuwa na umuhimu mkubwa kwetu kwani tunanuia kuchunguza taswira, nafasi

na utambulisho wa mwanamke katika tamthilia, sawa ya Mirikau. Hata hivyo, utafiti wetu utahusu nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani*, tamthilia za Kithaka Wa Mberia. Ingawa mhakiki huyu anatumia nadharia ya Ufemenisti wa Kiafrika kama sisi, tutapiga hatua moja zaidi kuangazia changamoto zinazowakabili wanawake katika harakati zao za kujikomboa.

Kazi nyingine itakayotufaa sana ni yake Onyoni (2012). Mhakiki huyu naye anachunguza usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala* na *Mama Ee.* Mhakiki mwenyewe anachunguza namna ambavyo mwanamke amesawiriwa katika kazi yenyewe. Tofauti na kazi hii, tutapiga hatua zaidi kwa kuangazia changamoto zinazosababisha hali yenyewe kama zinavyojitokeza katika tamthilia za Kithaka wa Mberia.

## 1.8 Njia za Utafiti

Utafiti wetu kwa kiwango kikubwa utakuwa wa maktabani. Tutasoma kazi zenyewe, kwa msingi wetu wa uhakiki. Pia tutasoma vitabu na maandishi/makala zingine zinazoangazia masuala ya kijinsia na hasa zile zinazozingatia Nadharia ya Ufeministi.

Pamoja na hayo, tutawashirikisha wahadhiri wetu, wataalamu wa fasihi pamoja na wanafunzi wenzetu katika mijadala, pamoja na kutaka ushauri wa kila itakapohitajika.

# SURA YA PILI

## NAFASI NA UTAMBULISHO WA MWANAMKE KATIKA *NATALA*.

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumechunguza nafasi na utambulisho wa mwanamke katika tamthilia ya *Natala* (1997). Katika uchunguzi wenyewe, tumeweza kutambua nafasi mbalimbali anazopewa mwanamke katika jamii. Tumebainisha nafasi zenyewe katika vitengo viwili: nafasi dhalilishi na dunishi na nafasi chanya.

Katika sehemu ya kwanza, tumebainisha nafasi dunishi na dhalilishi anayopewa mwanamke katika jamii kulingana na *Natala***.** Katika jamii yenye taasubi ya kiume, mwanamume huenziwa na mwanamke kudunishwa. Mwanamke mwenyewe huchukuliwa kuwa chombo cha kumfurahisha mwanamume, kiumbe duni asiyeweza kumiliki chochote, mtegemezi wa mwanamume kiuchumi, mtu mwovu, mgomvi na mtu asiye na shukrani , mbeya na msaliti anayetosheka na hali yake. Haya yote yamebainishwa katika sehemu hii.

Katika sehemu ya pili, tumeangazia nafasi chanya anayopewa mwanamke. Mwandishi amemjenga mwanamke kihadhi na kumwinua katika jamii inayomdhalilisha na kumdunisha. Hivyo, amedhihirisha nafasi chanya anayostahili kupewa mwanamke katika jamii inayozingatia haki na usawa wa kijinsia. Hivyo basi, sehemu yenyewe imeangazia nafasi chanya. Mwandishi mwenyewe amempa mwanamke nafasi hii chanya katika kubainisha na kuchochea mwamko wa wanawake. Hivyo basi,

amebainishwa katika tamthilia kuwa mtu jasiri, mlezi mwema, mwerevu na anayestahili uhuru wa kimawazo.

Katika sehemu ya tatu, tumetoa hitimisho la sura yenyewe Hapa , tumeangazia hoja muhimu zinazojitokeza kutokana na nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala*.

**2.1 Nafasi dhalilishi na duni ya mwanamke**

Suala la usawa wa kijinsia limepewa nafasi muhimu katika *Natala.* Mwandishi ameangazia ukinzani wa kimtazamo uliopo kuhusu nafasi sya mwanamke katika jamii.Taasubi tunayochorewa na mwandishi inadhihirisha mfumo ambao umejengeka na kudumu katika mila na desturi baguzi katika jamii. Mtazamo wenyewe unadhihirika kuwa ni wa ki-ubabedume, unaomkweza mwanamume na kumtweza mwanamke. Mila na desturi hizi zimewafanya wanaume kufikiria na kuamini kuwa wao ni bora kuliko wanawake.

Millet (1969:20) anapinga malezi yanayorutubisha na kudumisha ukinzani na ukandamizwaji wa mwanamke. Millet anaeleza namna ambavyo mtoto wa kiume hulelewa kwa namna ya kumwandaa kuwa mwanamume 'kamili' mwenye udhibiti na anayetumia nguvu kujikidhia haja zake za kiume. Millet anaelezea namna ambavyo mtoto wa kiume, katika jamii ki-ubabedume, huonea fahari kiungo cha kiume na kuchukulia kama silaha ya kuwanyanyasa wengine. Kiungo chenyewe huchukuliwa kama taashira ya 'uwezo' wa mwanaume. Katika *Betrayal In The City*

*(1976:13*), mhusika Mulili anaonyesha mawazo kama hayo. Anamdadisi mwenzake Jere kuhusu haja ya kunyenyekea mbele ya wahusika Doga na Nina. Anamwambia Jere, *wakati mwingine, najiuliza ni kwa nini unamiliki kiungo hicho, katikati ya miguu yako.*TY

Kithaka wa Mberia amefaulu kutusawiria picha ya jamii mojawapo ya Kiafrika inayotawaliwa na mfumo wa kiume. Katika *Natala* mwandishi amedhihirisha namna ambavyo mwanamume humchukulia mwanamke kama kiumbe duni, mtegemezi asiyejiweza kimaisha. Ameonyesha namna ambavyo mwanamke hutumika kama chombo tu cha kumhudumia na kumfurahisha mwanamume.

### 2.1.1 Mwanamke Kama chombo cha kumfurahisha mwanamume.

Millet (1969:20 ) katika harakati zake za kupinga nafasi chukivu ya mwanamke katika kazi za sanaa zilizoandikwa na waandishi wanaume kama Jean Genet , anadhihirisha namna mwanamume anavyolishughulikia tendo la ngono kama ishara ya udhibiti na uwezo juu ya wengine (wanawake). Anaangazia kazi ya Jean Genet, *The Thiefs Journal* na anafafanua mtazamo wa mwandishi aliyemwumba mhusika Armand. Mhusika Armand anajivunia na kuonea fahari ushindi wake kwa mwanamke ambaye ni kijakazi wake. Armand ananasibisha kitendo cha ngono na udhibiti, uwezo wake na ushindi.

Katika *Natala,* mwandishi anafaulu kutusawiria hali kama hiyo katika jamii hii aliyoitungia kazi yake. Amewaumba wanaume wawili (Wakene na Mhudumu wa

Jengo la Ufuo) wanaomchukulia mwanamke kama chombo cha kumfurahisha mwanamume. Haya ni matokeo ya malezi kwa watoto wa kiume. Katika onyesho la pili, Wakene anaingia kwa Natala huku akiimba. Anapotaniana na Gane, anajigamba mbele yake Gane kuhusu uwezo wake wa kiume. Anamwambia Gane;

> *Laani ulimwengu uliokufanya*
> *kuwa binamu yangu.Hujui*
> *unachokosa.Mtambo, Ungepata*
> *fursa ya kujua kwamba Wakene*
> *ni mtambo wa umeme* (uk.12).

Mhudumu wa Jengo la Ufuo naye ( Maigizo ya Bala) anajivunia uwezo wake wa kiume. Anamweleza Natala namna anavyopendwa na wake zake hasa mke wake Nawira. Anamwambia Natala;

> *Uwezo huo bado umo mwilini mwangu.*
> *Nguvu hizo bado zinaishi katika damu*
> *yangu (Anacheka kicheko cha*
> *kujipongeza )* (uk.22).

Ni dhahiri kwamba, mwanamke huchukuliwa kama chombo cha kumfurahisha mwanamume. Mwanamume hutarajia mwanamke naye aweze kufurahi, ajitolee

kumhudumia mwanamume hadi aridhike. Tunamwona Mhudumu mwenyewe anavyomtongoza Natala. Akimwaambia;

*Nyoyo zetu zinaweza kuburudika*
*kidogo! Zinaweza*
*Kusherehekea maumbile!* (uk 22).

Matamshi ya mhusika huyu yanadhihirisha kuwa anamchukulia mwanamke kama kiumbe duni asiyestahili heshima. Tayari Natala amejieleza kwake kuwa amekwenda kuchukua maiti ya marehemu mume wake. Kijamii, huyu ni mwanamke anayestahili heshima wala si kutazamwa kama kifaa cha kutumiwa na yeyote kama chombo cha kuzimia ashiki zake za kiume. Kwa hivyo, anakosewa heshima kwa sababu ni mwanamke, kiumbe duni. Anapokataliwa na Natala, anajiweka tayari kumrukia Natala. Anamjibu hivi, *Kazi bure , Moto utazimwa.Leo utajua mimi ni mwanamume halisi* (uk.22).

Kauli hizi zinadhihirisha namna jamii inavyotawaliwa na taasubi ya kiume. Jamii yenyewe humlea mtoto wa kiume kwa namna ya kumwandaa kutumia nguvu ili kudhihirisha uume wake. Mhusika mwenyewe anasema ‘Leo utajua mimi ni mwanamume halisi’ yaani kutumia nguvu kunaashiria uanaume.
Malezi ya mtoto wa kiume, anavyoeleza Millet (1969::20) humfanya kunasibisha uume na matumizi na nguvu, utundu na umilikaji wa kila kitu. Anasema kuwa malezi haya

humfanya mwanamume kutumia kiungo cha kiume kuwanyanyasa watu wengine (wanawake).

Wanawake nao wanaonekana kuwa wamedanganyika kiasi cha kuamini kuwa wao ni vyombo vya kumfurahisha na kumridhisha mwanamume. Mama Lime anaamini kuwa wake zaidi ya mmoja huhakikisha kwamba, mwanamume anaridhika. Anamweleza Natala kuwa mababu wa zamani walikuwa werevu. Kwamba walihakikisha kuna ushwari katika familia kwa kuanzisha ndoa za wake wengi, ili wanaume waridhike. Kwa hivyo , Mama Lime anamtaka Natala arithiwe na Wakene, kwani ingekuwaa na manufaa kwake na Wakene. Natala anapinga vikali mtazamo kama huu kwani unalenga kumpendeza mwanamume na kumpuuza mwanamke.

**2.1.2 Mwanamke kama kiumbe duni asiyeweza kumiliki chochote.**

Jamii nyingi na hasa za Kiafrika, bado zinashikilia tamaduni au mfumo unaomwenzi na kumkweza mwanamume huku ukimtweza na kumdhalilisha mwanamke. Greer (1970:1) anapinga asasi za kisiasa na za kiuchumi ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikitumiwa kumdhalilisha mwanamke katika jamii. Kiuchumi, mwanamke huchukuliwa kama mtegemezi asiyezalisha mali. Badala yake anaonekana kuwa yeye humletea mwanamume mzigo kiuchumi. Kutokana na mtazamo unaotokana na taasisi hizi, wanaume hujiona kama wanadamu vielelezo, wenye vyeo, heshima na hadhi kubwa kuliko wanawake. Greer anaangazia hali inayowakabili wanawake, hasa wanaoishi vijijini. Wanawake kama hawa aghalabu

huwa hawana miungano. Kwa hivyo, huishia kuwa wategemezi kwa waume wao kielimu, kihisia na hata kiuchumi.

Mwandishi huyu amefaulu kudhihirisha hali hii katika *Natala*. Amebainisha nafasi anamowekwa mwanamke kiuchumi kupitia wanayoyasema na wanayoyatenda wahusika wanawake. Katika onyesho la kwanza, mwandishi anamtumia mhusika Tila kutuonyesha nafasi ya mwanamke kiuchumi. Kwamba hana chochote anachomiliki bali mali yote ni mwanamume. Tila anapoelekezwa na Natala aondoke kwake, anasema, *Niko kwa kaka ya mume wangu*. (uk.5)

Matamshi yenyewe yamelengwa kumwelekeza Natala afahamu kuwa hana chochote kwani mali yote ni ya mume wake ambaye ni Tango Mwina. Anadhihirisha namna ambavyo wanawake wamelelewa katika jamii ya ki-ubabedume na wakawa wamerengwa kukubali kuwa wao ni wasaidizi tu lakini anayemiliki kiunzi cha kuzalisha mali ni mwanamume. Kwamba, mwanamke hutumika tu kama chombo cha kumzalishia mali mwanamume lakini hawezi kumiliki mali yenyewe. Natala amechangia pakubwa katika kuzalisha mali . Lakini anakumbushwa kuwa mali ni ya kakake mumewe yaani Tila.

Katika uigizaji wa yaliyotukia katika Jengo la Ufuo, Bala anayemwigiza Mhudumu wa Jengo la Ufuo, anadhihirisha nafasi anayowekwa mwanamke kijamii. Kwamba huwekwa katika nafasi duni. Anapoisemesha maiti, analinganisha hali

yake na mwanamke. Anaisemesha, *Wewe! Usilale kipumbavu Kama mwanamke* (uk.19).

Mwanamke ananasibishwa na hali duni ya upumbavu. Kwa hivyo, chochote au yeyote anayedhihirisha upumbavu hunasibishwa na mwanamke. Natala anapohoji maoni yenyewe, anakumbushwa kuwa mwanamke aliumbwa kutoka kifupa cha mwanamume kwa hivyo si sawa na mwanamume. Anakumbushwa kuwa hakuna chochote kinachomfanya mwanamke kuwa sawa na mwanamume. Kwamba nafasi yake ni chini ya mwanamume 'Kimaumbilie'. Mwanamume hutafuta sababu ya kumweka mwanamke katika nafasi ya chini. Kwamba, kulingana na Biblia imekuwa hivyo tangu mwanzo.

Jamii nyingi za Kiafrika, ikiwemo iliyotungiwa tamthilia hii zinatawaliwa na mfumo wa kiume au ki-ubabedume unaomchukulia mwanamume kama mdhibiti wa kiuchumi huku mwanamke akichukuliwa kuwa msaidizi tu, asiyeweza kumiliki chochote. Beauvoir (1949:114) anatoa fasili ya umilikaji huu wa mali. Anaeleza namna ambavyo mwanamke huchukuliwa kuwa mali ya mwanamume na hivyo kumilikiwa tangu utotoni: azaliwapo huwa mali ya babake na baada ya kuolewa humilikiwa na mumewe. Beauvoir anapinga hali inayomchukulia mwanamke kama kiumbe duni. Badala ya kumiliki mali, ni yeye anayemilikiwa. Katika *Natala*, anatusawiria jamii ya ki-ubabedume. Mwanamume angependa kurithi mali ya marehemu, pamoja na mkewe. Anapokataliwa, anaamua kurithi mali yote na watoto wabakie katika familia ya marehemu. Wakene anasema;

*Na kwa sababu wewe mwenyewe*

*umeamua kujitenga na familia*

*yetu……… kaka yangu aliacha*

*shamba na nyumba.Mali hii haina*

*budi kubakia kwenye familia yake (*uk.52).

Wakene anamweleza Natala yaliyomleta kwake. Kwamba ni haja ya kuchukua cheti cha shamba na kumjulisha Natala akatafute mahali pa kuhamia peke yake kwani watoto watabakia katika familia ya marehemu Tango .Maamuzi haya yanadhihirisha jinsi jamii inavyomwona mwanamke kuwa kiumbe duni asiyeshauriwa. Hutarajiwa kufuata maamuzi ya mwanamume bila kupinga. Wakene anatarajia Natala afuate uamuzi wenyewe bila kupinga. Natala anakosewa heshima kwani haki zake zinakiukwa. Licha ya hayo, anapewa ilani na kunyakuliwa kwa haki ya umilikaji wa shamba. Huku ni kumkosea heshima. Hali hii inamkabili Ramatoulaye, katika *So Long A Letter* (1980:10). Ramatoulaye alikuwa amechanga ujenzi wa nyumba, na mumewe. Lakini mumewe akajiandikia kama miliki yake. Hivyo, Ramatoulaye anasononeka kwa namna mumewe, Modou alitumia mkopo wenyewe kumjengea mamake nyumba. Ramatoulaye mwenyewe anaamua kumwaga dukuduku lake kwa shogake, Aissatou. Anafanya hivi katika hatua ya ‘kujitibu’.

### 2.1.3 Mwanamke kama mtegemezi wa mwanamume

Kithaka wa Mberia anabainisha nafasi anamowekwa mwanamke katika jamii kiuchumi. Anadhihirisha namna ambavyo malezi ya jamii yamemtenga mwanamke kwa kuamini kuwa hali yake ni ya utegemezi kiuchumi, kijamii na hata kimawazo. Mwanamke, hivyo basi, anaamini kuwa anahitaji mhimili ili kufaulu maishani. Akitoa mfano wa uchunguzi uliofanyika katika kiwanda kimoja cha Renault , Beauviour (1969:690) anafafanua hali ambapo wanawake wengi wamebakia katika ngome zao za nafsi . Kwamba hawa hawajajikomboa kiakili. Desturi za kike zinawagubika na kuwafanya watosheke kiuchumi na kijamii katika hali duni kimaisha. Haya yamedhihirishwa na mwandishi huyu, Kithaka wa Mberia ambaye amemwumba mwanamke anayetosheka na hali duni. Huyu ni mhusika Mama Lime. Haamini kuwa mwanamke anaweza kujitegemea, akajimudu kimaisha. Hivyo, anapotumwa na wazee wa ukoo, anapeleka ujumbe wenyewe kwa Natala. Ujumbe wenyewe unahusu kurithiwa kwa Natala baada ya Tango ‘kuaga dunia’. Mama Lime mwenyewe anamwelezea Natala kuwa, *Njia nzuri ya kuwalea bila shida ni kushirikiana na mwanamume. Unahitaji usaidizi.* (uk.36)

### 2.1.4 Mwanamke kama mtu mwovu

Wanjiku na Akinyi (1993:13), katika uchunguzi wao kuhusu hali ya mwanamke barani Afrika na mchango wa makundi ya wanawake, walitambua kuwa, jamii nyingi zimemtenga mwanamke na nafasi muhimu katika jamii. Walitambua kuwa jamii nyingi za Kiafrika humnasibisha mwanamke na maovu katika jamii. Kwamba nafasi za uongozi na za kiuchumi hudhitibiwa na mwanamume. Mwanamke

hashirikishwi kwa sababu ya kuhusishwa na dosari na maovu. Kithaka wa Mberia naye amesawiri nafasi hiyo kwa kuhusisha baadhi ya wahusika wake wa kike na maovu ya kijamii kama ugomvi, umbeya na usaliti

**2.1.5 Mwanamke Kama mgomvi na mtu asiye na shukrani.**

Kwanza, mwanamke amesawiriwa kuwa mgomvi na mtu asiye na shukrani. Hata atendewe fadhila za kiwango gani huishia kudharau na kukosa shukrani. Mhusika Tila anasaidiwa na Natala kwa kupewa sukari na mafuta ya taa. Na anapokwenda kuomba chumvi, anamgombanisha Natala kwa kukumbushwa fadhila zenyewe. Tila mwenyewe anadhihirika kuwa mtu asiye na shukrani, mgomvi na mwenye dharau. Anapogawiwa chumvi, anasema: *Umenipimia kama dawa ya mtoto*.(uk.3)

Licha ya hayo, anamdharau Natala kuwa yeye (Natala) si chochote si lolote kwani yeye (Tila) yuko kwa kakake mume wake. Anamdharua Natala kwa kumnyima chumvi ilhali hamiliki chochote humo. Na kwamba mali aliyo nayo ni ya Tango Mwina, si yake yeye Natala.

**2.1.6 Mwanamke Kama mmbeya.**

Mwandishi amemsawiri mwanamke kuwa mtu mbeya. Mhusika Tila, kwa mfano , anamwendea Natala kwa ghasia huku akidai kuwa ana habari kamili kuhusu mipango ya Natala na Mama Lime, ya kumnyakua Wakene.Anafika kwa Natala na kumdadisi kuhusu ‘hatua’ zake. Anamwambia,

*Taratibu! Twende taratibu! (Kimya kifupa)*

*Labda ulidhani sijui. Kujua ninajua, tena*

*Vizuri Sana. Na si Mimi pekee.Wengine*

*Wanajua* (uk.42).

Msomaji na Natala wanafahamu kuwa huu ni umbeya usiokuwa na ukweli wowote. Lakini unaosambaratisha itifaki nzuri na mlahaka mwema katika jamii. Tila anamwelezea Natala kwamba anafahamu namna Natala mwenyewe alivyomlilia Mama Lime na kumpa ahadi ya kulipwa endapo angefaulu kumshawishi Wakene akamrithi Natala mwenyewe.

Zaidi ya Tila , kuna mwanamke mwingine mbeya aliyesikika akieneza fitina juu ya mustakabali wa Bwanu na Alika , watoto wa Natala. Mama mwenyewe alisikika akieneza umbeya kwamba Bwanu hangesoma na kwamba Alika hangeendelea na masomo. Badala yake angefanya kazi katika vilabu vya pombe.

Huu ni umbeya unaoharibu mtagusano na uhusiano mwema katika jamii. Uozo wenyewe umenasibishwa na mwanamke.

**2.1.7 Mwanamke kama msaliti anayetosheka na hali yake**

Mwandishi huyu pia amefaulu kujenga picha chanya ya mwanamke kijamii. Mwanamke badala ya kushirikiana na wanawake wenzake ajiinue na ajikakamue na ajijenge kihadhi, anamsaliti mwenzake.Anashirikiana na adui wa mwanamke mwenzake.Kithaka wa Mberia amemuumba mhusika wa aina hii. Umri wa Mama

Lime na tajriba zake zinatosha kumbadilisha kuwa mshauri na mpatanishi katika masuala ya kijamii na ya kinyumbani. Lakini anayoyasema na kuyafanya ni kinyume na matarajio yetu. Anashirikiana na Wakene kumyanganya Natala haki yake.Anamwelekeza Wakene achukue karatasi yenyewe (cheti cha kumilikia shamba).

Anamwambia, *basi unangojea nini? Nenda ukachukue* (uk.53). Bala na Gane wanapoingilia kati, ndiye anayewaonya dhidi ya kuingilia mambo ya nyumbani. Huyu ni mwanamke anayesaliti hatua za kumkomboa mwanamke na hivyo, kukwamiza ufanisi wenyewe. Badala ya kuleta uwiano na kuwapatanisha Wakene na Natala kuhusu ugavi wa mali, anaegemea upande wa Wakene na kumchochea achukue hatua dhidi ya Natala.

**2.2 Nafasi chanya anayopewa mwanamke katika jamii.**

Mwandishi anaangazia uwezo na mchango muhimu wa mwanamke katika ujenzi wa jamii mpya. Zaidi ya kuonyesha taswira chanya, anadhihirisha uwezo na nguvu za mwanamke ambazo zikiimarishwa, zitakuwa msingi muhimu katika jamii yenyewe. Kwamba zitahakikisha usawa na haki kwa jinsia zote mbili.Hili ni jambo linaloangaziwa vyema.

Kama njia mojawapo ya kusisitiza haja ya kumkomboa mwanamke katika jamii, amemwumba mwanamke jasiri, huru kimawazo na mlezi mwema. Akamfanya kuwa mhusika mkuu hadithini. Huyu ni Natala anayetumika kama kielelezo cha

kuendeleza harakati za ukombozi wa mwanamke katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa kiume. Anafanya hivyo kwa nia ya kuitafakarisha jamii razini na hasa wanawake kuhusu haja na namna ya kujinyakulia ukombozi wao.

Wanjiku na Akinyi (1993:1) wanatoa pendekezo kuhusu suala la usawa wa kijinsia .Kwamba, wanawake kwa wanaume wanastahili kujitahidi kwa ushirikiano katika kupiga vita ubabe-dume katika jamii. Wanaelezea kwamba, maumbile hayawezi kubadilishwa lakini mfumo unaweza kubadilishwa kwa sababu ni tokeo la jamii la Mazoea na desturi. Kwao, jamii inaweza kubadili mfumo ulioanzishwa na wanajamii wenyewe.

Kwa maoni yao, kile kilichoanzishwa na jamii kinaweza kubadilishwa na jamii iyo hiyo. Msanii Kithaka wa Mberia ametumia sanaa yake kumwinua mwanamke kihadhi na kuizindua jamii kuhusu haja ya kutambua mchango muhimu wa mwanamke katika jamii kwa ujumla. Nafasi anayompa Natala tamthiliani inalenga kudhihirisha kuwa jamii itafaulu kubadili mkondo wa mambo endapo wanawake na wanyonge watajasiria na kupinga mazoea na desturi zinazowakandamiza na kuwatweza.

### 2.2.1 Mwanamke kama mtu Jasiri

Kithaka wa Mberia amefaulu kumsawiri mwanamke wa kisasa, mwenye ujasiri mwingi katika tamthilia ya *Natala* . Mwanamke mwenyewe, Natala anasimama tisti na kuzikabili hali mbalimbali kwa ukakamavu bila kukata tamaa. Hatetereki katika hali

zozote zinazomkabili katika tamthilia. Beauvoir (1949:737) anafichua pingamizi zinazokwamiza ufanisi wa kumkomboa mwanamke. Mojawapo ni mwanamke mwenyewe kuangalia nyuma katika maisha. Kwamba wanawake watazame mbele na kujikaza vilivyo. Natala anaonekana kufanya hivyo kwani anasabilia kuvunja 'desturi na mazoea' katika jamii ya ki-ubabedume. Anajitokeza kuwa kielelezo cha vita dhidi ya uhafidhina na mazoea.

Kwa mfano anapofika katika Jengo la Ufuo (maigizo yake na Bala), anamkabili mhudumu mwanamume anayedhihirisha taasubi ya ki-ubabedume. Natala anamsemesha kwa ujasiri mwingi. Picha tunayopata ni ya mwanamke wa kisasa, aliyejikomboa kiakili. Si mwanamke mtamaduni tena. Tofauti na wanawake wengine kama Mama Lime wanaoendeleza uhafidhina, Natala anavunja 'kawaida'. Anamsaili mhudumu mwenyewe anayesemesha maiti kwa namna ya kumdhihaki mwanamke. Natala anamwuliza, *Mwanamke hulala vipi?* (uk. 19)

Kwa Natala, haya ni matusi kwani mwanamke si mpumbavu wala si gogo la mgomba. Anamzindua kwa ujasiri kuwa mwanamke ni binadamu. Mhudumu mwenyewe anajitetea kwa kurejelea maandiko, kwamba mwanamke aliumbwa kutoka kifupa cha mwanamume. Huyu ni kiwakilishi cha ubabe-dume na hivyo, anatoa fasili ya nafasi anayopewa mwanamke katika jamii yenye ubabe-dume. Maelezo yake yanamwudhi Natala, anayetambua kuwepo nafasi sawa ya mwanamke na mwanamume katika jamii 'huru.' Kwa hivyo, anamtazama mwenzake kwa macho ya bezo.

Ujasiri wa Natala pia unamfanya apinge vikali ufisadi unaoendelezwa na baadhi ya wanajamii. Anapotambua dalili za kuitishwa hongo, amkabili mhudumu huyo kwa dhati. Anamwambia;

> *Unalipwa kila mwezi, kila mwisho wa mwezi!*
>
> *Fanya kazi uliolipwa kufanya. Nipe maiti*
>
> *niondoke.* (uk. 22)

Kauli hiyo inamghairisha mwenzake kufikiria namna ya kulipwa kwa huduma zake. Anaanza kumtongoza. Lakini Natala anamzindua. *Mimi si mlango wa jengo la umma kuguswa na kila mtu.* (uk. 22)

Matamshi kama haya yanatolewa na mhusika Ramatoulaye katika *So Long A Letter (1980:60).* Anamwambia Tasmir, nduguye mume wake Modou. Tasmir anataka kumrithi Ramatoulaye baada ya Modou kuaga dunia. Lakini Ramatoulaye anamkemea kwa kumwambia, *mimi si kifaa kinachoweza kuhamishwa kutoka mkono mmoja hadi mwingine* (1980:60).TY

Huyu mwanamume anashindwa "kumshawishi" Natala, ndipo anaazimia kutumia nguvu. Hii ni ishara ya kushindwa, na inayochukuliwa na wanaume wenye taasubi ya kiume. Kwao, matumizi ya nguvu ni udhibiti. Huwawezesha wengine watambue kuwa wao ni wanaume halisi. Lakini Natala hatishiki. Badala yake anakabili vitisho kwa kutoa vitisho vyake. Anamwambia, *Na wewe utajua mimi ni binadamu kamili.* (uk. 22)

Mhudumu mwenyewe anatambua huyu ni mwanamke asiyetetereka. Anapomrukia Natala, anaangushwa na mwanamke mwenyenye. Hii ni taashira anayodhihirisha mwandishi kwani tunaona mwanamume akiangushwa na mwanamke jasiri aliyejikomboa. Mwandishi anawatafakarisha wanawake kuwa ujasiri wao utaangusha ubabe-dume uliokita mzizi katika jamii. Ni kama anawahimiza kuendeleza ukakamavu na bila shaka watafaulu kuporomoa ubabe-dume.

Baada ya uigizaji wa yale yaliyomkumba Natala katika Jengo la Ufuo, Natala anapongezwa kwa ujasiri na kwa kuhifadhi heshima yake. Ni ujasiri uliomkomboa Natala pale Ufuoni. Mwandishi anawahamasisha wanawake wapiganie haki yao kwa kuwa kuna wanaume wanaowaunga mkono. Amemjenga mwanamke kihadhi kwa kumpa mhisani anayempongeza, kwa jina Bala.

Natala pia anadhihirisha ujasiri anapoamua kukabiliana na hali na maisha ya ujane kiume. Tofauti na wanawake wengine, anakataa katakata kurithiwa na Wakene nduguye Tango. Kwanza anajiona kuwa mhimili katika familia yake. Katika mazungumzo yake na Gane, anawasikitikia watoto wake kwani *"… hawajui kuwa kutoka sasa hawatakuwa na mikono miwili ya kuwahimili"* (uk 23). Hataki mhimili mwingine kwani anaoina kuwa anatosha kukabiliana na hali yenyewe liwe liwalo. Anamwambia Mama Lime kuwa yeye (Natala) atapita 'njia nyingine' wala si ile ya kurithiwa. Kwa hivyo, anamtuma Mama Lime akawaelezea wazee wa ukoo kuwa yeye ni binadamu wala si kifaa.

Wakati wa mazishi (onyesho la III), Natala pia anavunja "mazoea" kwa kupinga ufisadi katika jamii. Ni mazoea kwa sababu tunaona kwamba, aghalabu katika kila hatua ya kumhudumia mwanajamii hadithini, mtoaji wa huduma yenyewe anataka kupewa hongo. Tunamwona Chifu 'akilegeza' msimamo kwa kukubali mazishi yaendelee lakini kwa masharti kuwa Mzee Balu aende kwake akipata 'nguvu'. Yaani atakapopata pesa amlete Chifu kwa sababu Natala anakataa kumpa. Wanaoomboleza walipoarifiwa kuhusu ujumbe wa Chifu, Natala anatoa kauli ya kuendelezwa kwa mazishi yenyewe. Anasema kuwa kufika kwa Chifu hakutabiriki kwani huenda akachelewa. Chifu anapofika anatishia kuchukua hatua ili kuhakikisha mazishi yanasitishwa kama 'adhabu'. Anakabiliwa vilivyo na Natala anayemwambia,

> *Bwana chifu, mimi ni adui mkubwa*
> *wa mambo hayo. Moyo wangu*
> *unayapinga sana* (uk.32).

Tayari, alikuwa amekabiliana na kina Tila, Wakene na Mama Lime alipopendekeza jeneza lisifunguliwe. Sababu anayotoa ni kwamba uso wa marehemu ulikuwa umepondeka sana. Ingawa wanampinga vikali, Kasisi anafuata matakwa ya mke wa marehemu. Sawa na Mzee Balu anayemuunga mkono 'mwanamke', Kasisi anatambua na kumheshimu Natala. Wakene anamsaili Mzee Balu na kumwuliza Natala, *Huelewi niyasemayo? Kwa nini una kiburi hivi?* (uk.29)

Wakene anachukulia ujasiri wa Natala kuwa ujeuri na hivyo, kumdadisi kwa namna inayodhihirisha kutamauka kwake kumdhibiti mwanamke huyu. Anatoa vitisho.Hatambui kuwa Natala si mwanamke wa kutishiwa akatishika.

Mwandishi anamwumba mwanamke kielelezo kama mchango wake wa kuijenga jamii yenye usawa na inayoendeleza na kuhimiza maadili mema katika jamii. Miongoni mwa wahusika wote anaowaumba, ni Natala peke yake anayechukua hatua kupiga vita uozo wa kijamii kwani kizazi cha kale huenda kikaudumisha uhafidhina. Na anayemtumia ni mwanamke wa makamo, Natala. Natala mwenyewe anamdadisi Mzee Balu kuhusu 'masharti' anayoyatoa Chifu. Anapogundua ni hongo, anamzindua Mzee Balu kuwa, *Usiende huko Baba! Usikubali kuutilia ugonjwa wa ufisadi mbolea* (uk.33). Mzee Balu mwenyewe anamweleza Chifu kwamba yeye hana nguvu na hivyo, Chifu anasema mazishi yaendelee lakini Mzee Balu amwendee punde atakapopata nguvu. Mzee Balu mwenyewe anapozungumza na Chifu anasema kuwa Natala ni 'mgumu'. Anafahamu ujasiri na ukakamavu wa Natala.

Katika onyesho la V, Wakene, Mama Lime na Mzee Palipali wanamwendea Natala wakiwa tayari wamejipanga kumfunza adabu. Wanatarajia kumpa adhabu Natala kwa kukataa kuitikia matakwa yao. Adhabu yenyewe ni kuchukua cheti cha kumiliki shamba na kumfurusha Natala mwenyewe. Lakini inawawia vigumu kumkabili mwanamke huyu. Mama Lime anatangulia na hivyo anahojiwa na Natala kwa ujasiri kuhusu mipango ya kurithiwa Natala, awe mke wa pili Wakene. Hayo yanajiri baada ya Tila kumwemdea na kumgombeza Natala. Siku hiyo asubuhi wakene na Mzee Palipalali nao waliingia baadaye. Wote watatu wanashindwa kuanzisha mazungumzo yenyewe. Ni baada ya mazungunzo kuendelezwa ambapo Wakene anakabiliwa na mwanamke huyu jasiri. Anamwambia, *Wakene, umerukwa na akili!*( uk. 53)

Anamkumbusha Wakene kuwa ndoto zake za kupata mali kwa urahisi hazitafaulu (uk. 53). Wakene anaamua kutumia nguvu lakini Natala anamkabili mwanamume huyo vikali. Mvutano wenyewe unaendelea kwa muda, kabla ya Wakene kutoa vitisho. Vitisho vyenyewe havimshtui Natala. Bado anamkumbusha Wakene kuwa**,**

> *… bila shaka mimi ni mwanamke.*
> *Lakini utagundua kuwa sio kila*
> *Mwanamke. Hutetemeka mbele ya*
> *mwanamume.* (uk .53)

Anapotishwa tena, kwamba angetoa machozi endapo angekosa kumwachilia Wakene, anamwambia kuwa yeye Wakene angelia kabla ya Natala kulia. Mapambano yenyewe yanaafikiana na himizo la Greer (1970:9) kwamba unyanyasaji utaisha tu endapo mwanamke atasabilia kupigania haki yake ya kuwa huru na sawa na mwanamume. Greer anaonelea kwamba ni hadi wakati ambao mnyonge atachukua hatua hii ndipo unyonge utakapomalizika.

### 2.2.2 Mwanamke anahitaji na anastahili kuwa huru kimawazo.

Kithaka Wa Mberia anamsawiri mwanamke ambaye amejikomboa kimawazo. Natala ana mawazo huru yasiyoyumbishwa wala kutereshwa na kimbunga chochote. Wollstonecraft (1792) anawahimiza wanawake wasimame kidete na kupigania haki zao kwa ujasiri bila kuiruhusu jamii iwafafanulie kinachowafaa. Kwa Wollstonecraft, mwanamke ana uwezo wa kujiamulia na anastahili kufanya hivyo bila kuelekezwa na jamii. Mwanamke hafai

kuitegemea jamii katika maamuzi yake. Greer (1970) anaona kuwa jamii haielewi yanayomfaa mwanamke kama ambavyo mwanamke mwenyewe anavyoelewa. Naye Mogambi (1983:6) anaeleza namna mwanamke anavyobanwa na kupewa sifa za unyonge, asiye na nguvu wala uwezo mbele ya mwanaume.

Mama Lime anapotumwa na wazee wa ukoo kumpelekea Natala uamuzi wao kuwa arithiwe, Natala anakataa katakata na kusema kwamba, yeye atafuata njia nyingine. Natala mwenyewe si mwanamke wa kuelekezwa na mila au desturi kwani anayafahamu yale yanayomfaa na yale yasiyomfaa. Anashikilia uamuzi wake wa kukabiliana na maisha ya ujane kwa hivyo anamtuma Mama Lime akawaambie wazee wa ukoo kuwa *yeye ni binadamu wala si kifaa* (uk. 40).

**2.2.3 Mwanamke kama mlezi mwema wa watoto.**

Mwanamke pia anasawiriwa kama mlezi mwema wa watoto. Ni mtu mwenye mapenzi ya dhati kwa familia yake. Namna anavyowashughulikia wanawe na habari za kuja kwa Tango vinadhihirisha Natala kuwa mlezi mwema. Anatimiza wajibu wake kama mzazi hasa kwa wanawe Alika na Bwanu. Matamshi ya Gane yanadhihirisha kuwa Natala ni mlezi mwema anayefaa kuigwa. Gane anamwambia,

> *Mapenzi yako imara, moyo wako*
> *wa kazi na nidhamu yako thabiti ni*
> *baraka kubwa. Baraka hizi zitakuwa*
> *jahazi la kuwafikisha watoto wako*
> *waendako.* ( uk. 24)

Anawashughulikia watoto wake vilivyo kwa kuwalisha na hata kuwaelezea umuhimu wa kula vizuri kwani watapata nguvu za kukabiliana na magonjwa. Vilevile watakuwa wakubwa. Kwa hivyo, anawahimiza kila wakati wamalize vyakula wanavyoandaliwa. Pia, hataki chochote kinachoweza kuwasumbua wanawe kisaikolojia. Katika kuhakikisha kuwa hawaathiriwi na hatua yenyewe, tunamwona akipinga hatua ya kufungua jeneza. Kwake, hatua kama hiyo ingewatia 'jeraha la milele' watoto wake. Kwa hivyo, pendekezo lake linafuatwa na waombolezaji wanaohudhuria mazishi.

Licha ya hayo, anadhihirisha ulezi mwema kwa namna anavyoshughulikia mambo yaliyosemwa na 'mama mmoja'. Natala anamhakikishia mwanawe, Alika kuwa yote yatakuwa sawa kwao. Kulingana na Alika, mama huyo alisema kuwa 'Bwanu hatasoma' bali atakuwa kibarua katika mashamba ya majirani. Mama mwenyewe pia alisikika akisema kuwa Alika mwenyewe hangeendelea na masomo yake (uk.46). Natala mwenyewe anamhakikishia Alika kuwa masomo yao yangeendelea bila kukatizwa. Maelezo yenyewe anayatoa kwa mapenzi ya dhati bila kumwonyesha kuwa anaudhika kusikia hayo. Kwa hakika , habari kama hizo zinazoenezwa na mwanamke mwenziwe zinatarajiwa zimvunje moyo yeyote anayerejelewa. Lakini anayashughulikia maslahi ya wanawe kwa busara kubwa.

Zaidi ya hayo, tunamwona akiwaonyesha wanawe 'ukunjufu' hata wakati anapokabiliana na mahasidi na mahasimu wake. Katika onyesha la tano, anapokabiliana na akina Wakene, Mama Lime na Mzee Palipali, wanawe wanamwendea. Ingawa alikuwa

amekasirishwa na matakwa ya watatu hao, bado anawashughulikia wanawe kwa ukunjufu na mapenzi ya mlezi mwema.

### 2.2.4 Mwanamke kama mtu mkakamavu.

Kithaka wa Mberia anamsawiri mwanamke mwenye ukakamavu mwingi. Hadithini, inafikia hali ya kutamausha kwani Natala anakabiliwa na mambo mengi ya kusumbua akili na mawazo. Lakini bado anajikakamua kuyashughulikia yote. Tutamwona namna anavyojipiga moyo konde kumnyang'anya Wakene cheti cha kumiliki shamba. Hatamaushwi na hatua ya Wakene ya kwenda kuchukua cheti chenyewe wakati Natala anapowashughulikia wanawe. Anaporejea anafululiza moja kwa moja hadi chumba cha kulala na kupambana na mwanamume huyo. Mapambano yenyewe yanaendelea kwa muda. Natala mwenyewe hakati tamaa bali anajikakamua zaidi.

Hata pale ambapo watu wengi wangetamauka na kukubali kushindwa, Natala anashikilia msimamo wake. Wakene anamburura hadi sebuleni, anamchapa kofi, anamtisha. Lakini yote yanaambulia patupu kwani Natala ni mkakamavu asiyetamauka kwa urahisi.

Licha ya hayo, Natala anadhihirisha ujasiri na uelewa wake katika Jengo La Ufuo. Mhudumu anajaribu kila namna kumfanya atoe hongo lakini anashikilia msimamo wa kutoshirikiana na mafisadi kama mhudumu huyu. Hatimaye, Mhudumu anapojiandaa kumrukia, yuko tayari kujikinga. Bila kuhofia uwezekano wa kutopewa maiti, anangojea hadi mhudumu mwingine anapoingia. Huu ni ukakamavu wa hali ya juu.

### 2.2.5 Mwanamke kama mtu mwerevu.

Mwandishi amefaulu kumsawiri mwanamke kama mtu mwerevu. Werevu wenyewe umedhihirishwa na wahusika wanawake wawili: Natala na Mama Lime. Natala anadhihirisha werevu wakati anapotangamana na wanajamii wenzake. Kwa mfano, anapotangamana na Mhudumu katika Jengo La Ufuo, anamwuliza mhudumu mwenyewe chanzo cha kifo cha marehemu kakake. Majibu anayopewa yanamshtua. Kushtuka huku kunadhihirisha kuwa yeye anatambua chanzo chenyewe ( uk. 20).

Natala pia anadhihirisha werevu wake kwa namna anavyowalea wanawe . Kama mama mlezi, anatumia busara yake katika kutekeleza na kutimiza wajibu wake. Anawaelekeza wanawe kwa werevu wa kupigiwa mfano. Hata anapokasirishwa na wengine, hawaonyeshi wanawe kwamba amekasirika.

Licha ya hayo, anatambua kuwa Wakene ameingia katika chumba cha kulala. Anapoingia na kukosa kumwona ( uk.54) anatambua alikoelekea na anachokitafuta. Kwa hivyo, badala ya kuwasalimu Gane na Bala, anafululiza moja kwa moja hadi mle ndani.
Mama Lime naye anadhihirisha kuwa mtu mwenye busara wakati anapoongea na Natala. Kwanza, anagundua kuwa Natala amekasiririshwa na mtu fulani ( uk. 48). Anamwuliza, *Umekuwa ukiteta na nani?* (uk.48)**.** Maelezo anayompa Natala yanadhihirisha werevu wake. Anamwambia Natala kuwa ..… *mara nyingine masikio ya watu husikia kile yanachotaka kusikia.* Huu ni werevu kwani si watu wote wanaofahamu kwa nini kunatokea suitofahamu katika jamii. Lakini Mama Lime anaonekana kuelewa chanzo cha uvumi kama huo.

## 2.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangazia nafasi na utambulisho wa mwanamke katika jamii ya *Natala.* Tumeweza kubainisha nafasi anayopewa mwanamke katika jamii yenye mfumo wa ki-ubabedume. Jamii ya aina hii humwenzi mwanamume na kumtweza mwanamke. Kama wanavyoeleza Wafula na Njogu (2007:94) kuhusu mihimili ya nadharia ya Ufemenisti, washikilizi wa nadharia yenyewe wanapendekeza fasihi itumiwe kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo. Mwandishi amemsawiri mwanamke kwa namna ambayo amedhalilishwa na kudunishwa kwa kupewa nafasi chukivu kwa sababu ya mfumo wa ki-ubabedume. Haya tumeyaangazia katika sehemu ya kwanza.

Katika sehemu ya pili, tumetalii bayana nafasi chanya anayopewa mwanamke katika jamii. Mwandishi mwenyewe amefaulu kumjenga mwanamke kihadhi na kuonyesha mwamko wa mwanamke kupitia wasifu wa mhusika Natala. Kithaka wa Mberia ameitikia mhimili mojawapo wa nadharia ya Ufeministi. Mhimili wenyewe unajaribu kuwahamasisha wasanii kusana kazi zao kwa namna ya kuibua vielelezo. Wanaitifaki wenyewe wanapendekeza kwamba, wahusika wanaosawiriwa katika kazi za fasihi wawe wanaostahili kuigwa kimienendo na kitabia. Kwa hivyo, kwa maoni yetu, mwandishi huyu amefaulu kubainisha nafasi ya mwanamke na utambulisho wake katika tamthilia yenyewe.

# SURA YA TATU

# NAFASI NA UTAMBULISHO WA MWANAMKE KATIKA *KIFO KISIMANI*

## 3.0 Utangulizi

Sura hii, inashughulikia *Kifo Kisimani* (2001), tamthili ya Kithaka wa Mberia. Katika tamthilia yenyewe, tumekuwa tukichunguza iwapo mwandishi mwenyewe amefaulu kubainisha nafasi ya mwanamke na kumtambulisha katika jamii ya ki-ubabedume. Tumeainisha matokeo ya uchunguzi wetu katika makundi mawili makuu kama inavyobainika tamthiliani: nafasi dhalilishi na dunishi anamowekwa mwanamke- yaani, nafasi ya pili baada ya mwanamume na nafasi chanya kama anavyombainisha mwandishi kwa namna ya kumwinua na kumjenga mwanamke kihadhi tamthiliani. Mwishowe, tumetoa hitimisho la sura yenyewe kama ilivyobainika katika uchunguzi wenyewe.

## 3.1 Nafasi Dhalilishi na dunishi anayopewa mwanamke

Mwandishi amefaulu kubainisha nafasi dhalilishi na ya kudunisha anamowekwa mwanamke na jamii inayomwenzi na kumkweza mwanamume. Jamii ya aina hii ina mfumo unaompendelea mwanamume na kumtweza mwanamke. Kutokana na yale anayotendewa mwanamke, yanayosemwa kumhusu, anayoyasema na kuyafanya mwenyewe, mwandishi mwenyewe amebainisha nafasi hii dhalilishi na dunishi anamowekwa mwanamke. Kulingana na Wafula na Njogu (2007: 90), mwanamke amewekwa katika kitengo maalum katika jamii kwa sababu ya jinsia yake ya uke.

### 3.1.1 Mwanamke kama chombo cha kumfurahisha mwanamume

Kupitia matendo na maneno ya mwanamke mwenyewe, mwandishi amefaulu kubainisha nafasi anamowekwa mwanamke katika jamii ya ki-ubabedume.Mwandishi mwenyewe anadhihirisha namna ambavyo mwanamke mwenyewe amekubali hali yake na hivyo kujichukulia kuwa mtumbuizaji. Anahiari kumtumbuiza mwanamume na hasa kiongozi wa jamii. Batu anapokutana na Kaloo, wanajuliana hali. Baadaye ndipo Kaloo anamwelezea Batu kuhusu maandalizi ya matumbuizo ya Mtemi Bokono. Kaloo mwenyewe anasema, *Leo kuna mambo. Viuno vitatingishwa mpaka viyeyuke* (uk.3). Maelezo ya Batu yanadhihirisha namna ambavyo wanawake wenyewe wanavyowajibikia nafasi yenyewe. Anamwambia Batu, *Wanawake wa Butangi wasipomkatikia Mtemi; wamkatikie nani!*(uk.3)

Katika kumthibitishia Batu kuhusu maandalizi yenyewe, Kaloo anacheza ngoma mbele ya Batu. Minenguko yake hivyo basi, inamvutia mwanamume huyu. Naye anamhakikishia kuwa Mtemi atafurahia tumbuizo zenyewe. Na kwamba Mtemi akifurahi, nao wachezaji (wanawake) watafurahi na hasa kiongozi wa ngoma (Kaloo). Baadaye, katika Kisima cha Mkomani (uk. 90), tunamwona Zigu akimwelezea Kaloo namna Mtemi alivyomtaja mara mbili. Zigu mwenyewe anamwambia, *Jicho la Mtemi linaona; limekuona* (uk.90). Maelezo yenyewe yanadhihirisha kuwa Kaloo alikuwa katika kundi la waliomtumbuiza Mtemi katika mkutano wa Ilumbi. Mazungumzo yanayoendelezwa yanamdhihirisha mwanamke kuwa chombo cha kumfurahisha mwanamume. Kule kutajwa kwa jina la Kaloo kunadokeza malengo ya mwanamume ya kujifurahisha kimahusiano na mwanamke. Ni wazi kwamba, Bokono anataka awe na ‘uhusiano’ na

Kaloo mwenyewe. Tayari ana mke (Nyalwe) lakini bado anataka mwingine awe kimada wake. Kaloo mwenyewe anathibitisha haya anaposimulia namna Nyalwe 'alivyomparamia' mwanamke mmoja kwa kutuhumiwa kuwa hawara wa Mtemi Bokono. Naye Nyalwe anahofia kuwa huenda akaeleweka vibaya na Nyalwe mwenyewe. Bokono ana huyo hawara tayari anamtuma Zigu akamwitie Kaloo. Zaidi ya hayo, kauli ya Askari III kwake Askari I inadhihirisha mwanamke ni chombo cha kumfurahisha mwanamume. Askari II na Askari III wanapoanza kukimbilia usalama wao kutokana na umati unaoelekea gerezani, Askari I anawauliza yaliyojiri. Badala ya kumweleza hatari inayowakabili, Askari III anamjibu kuwa, *Mke wako anakuja. Anakuja kukuimbia nyimbo za mapenzi. Msalimie* (uk. 59).

Kutokana na ithibati hizi, mwandishi amefaulu kubainisha nafasi hii dunishi na dhalilishi anayopewa mwanamke.Na jinsi mwanamke alivyodanganyika akaiona hali hiyo kuwa ya kawaida. Kupitia Kaloo, mwandishi anabainisha 'kuridhika' kwa mwanamke kuwajibikia nafasi yenyewe. Ingawa ni nafasi dunishi, mwanamke mwenyewe anaonekana kutojali.

### 3.1.2 Mwanamke kama mmbeya

Nafasi nyingine duni anayopewa mwanamke, kama anavyobainisha mwandishi ni umbeya. Mmbeya ni mtu anayependa kupeleleza na kuzungumzia mambo yanayowahusu watu wengine. Nafasi hii imedhihirika katika tamthilia hii. Mwanamke ananasibishwa na umbeya mwingi. Nafasi hii inajitokeza wazi tamthiliani katika uhusiano baina ya wahusika wanawake wenyewe na wakati mwingine, mbele ya mwanaume. Mwanamke

mwenyewe anaonekana kufuatilia kwa undani mambo ya wengine, ambayo hayamhusu kwa vyovyote vile. Kaloo ni mmoja wa wanaojihusisha na umbeya huu. Katika mazungumzo na Atega, Kaloo mwenyewe anadhihirisha udaku wenyewe. Atega anapouliza iwapo Mwelusi amefika uwanjani, Kaloo anamwulizia moja kwa moja, *Mchumba wako atakuoa lini?* (uk.4). Kaloo anauliza swali lenyewe kwa namna inayodhihirisha kuwa habari zenyewe zimejadiliwa mahali. Swali lenyewe linamshangaza Atega na hivyo kumdadisi kuhusu chanzo cha habari zenyewe. Kaloo anathibitisha kuwa, *Wanawake wa kijiji chenu* (uk.5). Kaloo mwenyewe anazidi kumdadisi Atega kuhusu urafiki wao,yaani Atega na Mwelusi. Huu ni umbeya. Anasawiriwa kama mhusika anayepeleleza mambo ya wengine. Umbeya wenyewe unamshirikisha Azena. Azena mwenyewe anamthibitishia Atega kuwa tayari habari za 'uchumba' wao zimeenea kijijini pote. Anamwambia Atega kuwa *Watu wanasema kwamba yeye ni mchumba wako* (uk 5). Atega anawathibitishia kuwa uhusiano wao si uchumba. Atega anasema kuwa wanakutanishwa na maslahi ya jamii ya Wanabutangi.

Umbeya wa Kaloo unazidi kudhihirika anapokutana na Zigu katika Kisima cha Mkomani, Bonde La Ilangi. Kaloo mwenyewe tayari alikuwa amekwenda kwa Zigu, kwake lakini akamkosa. Akamfuata hadi kisimani. Lengo la Kaloo kumtafuta Zigu lilikuwa ni kumtuma Zigu akamshukuru Mtemi Bokono. Shukrani zenyewe zilihusu mwanawe Kaloo kuajiriwa kazi. Anamsimulia Zigu umbeya unaomhusu Nyalwe na mwanamke aliyeshukiwa kuhusiana na mumewe, Bokono. Kaloo anahofia uwezekano wa kueleweka vibaya. Anamwambia Zigu,

*Mkewe . Nasikia ni chui, kasoro*

*mkia na manyoya. Nasikia alimshambulia*

*mwanamke mmoja kwa meno na kucha*

*alipomshukuni hawara wa Mtemi.*

*Alipomaliza kumnyoa bila maji mwanamke*

*huyo alionekana kama alikuwa amenyeshewa*

*na mvua ya damu*. (uk.89)

Kwa hivyo, Kithaka wa Mberia amedhihirisha nafasi ambayo mwanamke amepewa katika jamii. Mwanamke ananasibishwa na umbeya na upelelezaji wa mambo ya watu wengine na kuyatangaza na kuyaeneza kijijini.

### 3.1.3 Mwanamke kama barakala.

Mwandishi huyu pia amefaulu kumbainisha mwanamke kama mtu mwenye tabia ya kujipendekeza kwa viongozi Ili kupata maslahi mbalimbali. Kupitia mhusika Kaloo, mwandishi mwenyewe amesawiri mtu anayemsifu kiongozi kwa lengo la kujifaidi. Kaloo anajipendekeza kwa Mtemi Bokono kupitia utumbuizaji anaouongoza ngoma ya wanawake wa Butangi kumwimbia Mtemi. Kutokana na hatua zenyewe, amefaulu 'kumshawishi' Bokono amtuze. Zigu anamwambia kuwa, *Jicho la Mtemi linaona; limekuona* (uk.90). Licha ya hayo, Kaloo mwenyewe anamtafuta Zigu ili amtume kwa Mtemi .

*Jambo la pili ambalo limenileta*

*ni kukutuma kwa Mtemi; Ningependa*

*umfikishie shukrani zangu za dhati.*

*Mtoto wangu amepata kazi ambayo*

*mtukufu Mtemi aliamuru apewe.*

*Hiyo ni hisani kubwa kwangu na*

*mtoto wangu.* (uk 89).

Mwanzoni mwa tamthilia (uk.6), tunamwona Kaloo akiwa na Azena wakimsifu na kumtukuza Mtemi na kuitikia mwito wa Batu wa kuonyesha ufuasi wao kwa uongozi wa Mtemi Bokono. Bila shaka, Kaloo mwenyewe anafanya hivi ili kujifaidi.

### 3.1.4 Mwanamke kama kiumbe duni asiyestahili heshima.

Kithaka wa Mberia amedhihirisha jinsi mwanamke anavyochukuliwa na wanajamii kuwa kiumbe duni asiyestahili heshima. Wamitila (2002:157) anaangazia madai ya Simone de Beauvoir (1953) kwamba, "mikabala ya kitamaduni inamwangalia mwanamke kama kitu hasi na kando huku ikimchukulia mwanamke kama kitu hasi na kando huku ikimchukulia mwanamume kama binadamu kielelezo''. Mawazo haya yanabainika wazi katika tamthilia hii. Mwanamke anadunishwa na kutendewa mambo yanayomfanya aonekane kiumbe asiyekuwa na usalama wowote. Kulingana na Wamitila (Khj), Beauvoir anaeleza kuwa utamaduni huchangia katika kumdidimizia mwanamke katika hali ya unyonge. Utamaduni unawafanya baadhi ya wanawake wanaishia kukubali na kuridhika na nafasi

wanayopewa katika jamii. Wengine hupinga kwa dhati hali yenyewe dunishi kama anavyodhihirisha, na kuna wale wanaokubali hali yenyewe bila pingamizi.

Wanaitifaki wa Ufeministi wa tapo la kimaeneo hasa eneo la Kiafrika, wanafafanua pingamizi zenyewe. Kulingana na wanaitifaki wenyewe, suala la utamaduni ni pingamizi kubwa katika kufanikisha usawa wa kijinsia. Kulingana na Wafula na Njogu (2007: 93), "Wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake." Miongoni mwa masuala wanayoyahoji waitifaki wenyewe kuhusu utamaduni ni kimya cha kulazimishwa. Si ajabu hivyo basi, kumwona mwandishi akipigia darubini hali yenyewe. Anadhihirisha namna suala lenyewe linavyozuia na kujenga ukuta baina ya hali ya 'utumwa' wa mwanamke na upatikanaji wa usawa wa kijinsia. Mwandishi amedhihirisha hali tofauti zinazobainisha ukweli kwamba, mwanamke hahitajiki kutoa kauli hasa kumpinga au kumshauri mwanamume. Nafasi yake ni kusikiliza na kutekeleza yale yanayoamuliwa na mwanamume. Bokono anaposhauriwa na hata kutahadharishwa na mkewe Nyalwe kuhusu uongozi mbaya, anaona kama Nyalwe mwenyewe anajaribu kumdunisha. Kwa hivyo, anajitia ukali na kumkemea akisema, *Sidanganywi! Na nyamaza!* (uk.16). Kwa sababu anayemshauri na kumpa tahadhari ni mwanamke, hayuko tayari kumsikiliza. Kwa hivyo, anamlazimisha anyamaze. Nyalwe alikuwa tayari kuchangia katika kuboresha uongozi huu lakini Mtemi hahitaji mchango wake.

Hata katika suala linalohitaji dharura, mchango wa mwanamke unapuuzwa. Baada ya kung'amua hali ya hatari, Nyalwe anahiari kumwendea mumewe na kumtahadharisha

dhidi ya kuvamiwa na waandamanaji. Lakini badala ya kutilia maanani maonyo yenyewe, Bokono anamnyamazisha Nyalwe. Bokono anaambiwa, *Usimkatishe Mtemi kauli katika Ukumbi wa Utawala!*(uk. 102*).* Hata anapohoji kuhusu mtu aliyekuwa akichapwa, anapuuzwa. Mwanamume huyu haamini kuwa mwanamke anaweza kutoa kauli zenye maana na ushauri wa manufaa. Kwa hivyo, badala ya kupoteza wakati kumsikiliza mwanamke, afadhali anyamazishwe.

Atega naye analazimishwa kuondoka, licha ya kunyamaza. Anakatazwa kueleza matatizo yake na Askari III. Badala yake anaamrishwa na mwanamke mwenzake, Tanya. Askari III anawaambia,

> *[kwa ujeuri] Ungependa, ungependa!*
> *Kwani wewe ni nani ufanye mambo*
> *unavyopenda? Wekeni vikapu chini na*
> *muondoke mara moja*! (uk. 56)

Sawa na Atega, Azena analazimishwa kunyamaza anapojaribu kumkaripia Askari III kwa sababu ya kumwangusha Tanya. Askari II anamkemea, *Nyamaza!* (uk.84).

Askari III anawakilisha taasubi ya kiume na wasioamini mwanamke anaweza kuwa sawa na mwanamume. Kwake, mwanamke anaweza kufanyiwa lolote. Andua anamweleza maagizo aliyopewa na mama kwamba, ahakikishe amempa chakula Mwelusi kwa mkono wake. Lakini Askari III anaona kama kupewa maelezo yenyewe ni kukosewa heshima.

Kwa hivyo, anaamua kumpa adhabu. Anamwambia Andua, *Usipoondoka, utatembelewa na kofi* (uk.35). Licha ya hayo, anajaribu kumgusa kifua chake. Huku ni kumkosea mtu heshima. Lakini kwa Askari III, hayo yanamfaa kiumbe huyu. Katika tukio jingine, tunamwona askari mwenyewe akipewa ushauri. Atega anamweleza kuhusu ubaya wa wa kuwa na ujeuri.Lakini Askari III anamtisha. Anamkemea, *Ngoja nitakuharibu sura!* (uk.56). Zaidi ya hayo, mwandishi amemtumia askari huyu kudhihirisha ubabe-dume katika tukio jingine. Askari mwenyewe anamwangusha Tanya kwa kutomjulisha alikoelekea mfungwa Mwelusi (uk 84).Wakati huo, Askari II na Askari III walikuwa wamekwenda kumtafuta mfungwa Mwelusi, aliyekuwa ametoroka gerezani.

**3.1.5. Mwanamke kama mtu mwenye hasira za mkizi.**

Kithaka wa Mberia amefaulu pia kubainisha sifa hii hasi ya mwanamke. Mwandishi mwenyewe anawaumba wanawake wanaodhihirisha hasira nyingi. Nyalwe na Tanya wametumiwa na mwandishi kudhihirisha sifa yenyewe. Nyalwe anamcharaza mwanamke mmoja aliyetuhumiwa kuwa hawara wa Mtemi. Haya tunaelezewa na mwandishi kupitia udaku wa Kaloo. Kaloo mwenyewe anaposhauriwa aende akamshukuru Mtemi, anakataa. Anasema sababu ni kuwa mkewe Mtemi ni mkali. Nyalwe anazidiwa na hasira kwa sababu ya mwanamke mwenzake anamnyemelea mumewe. Kwa hivyo, Nyalwe anamcharaza mwenzake huyo. Maelezo yenyewe yanamsawiri mwanamke huyu kuwa mwingi wa hasira.

Tanya naye anabainishwa na mwandishi kuwa mtu wa hasira. Haya yanadhihirika anapoudhiwa na mienendo ya mwanawe, Gege. Tanya mwenyewe anakasirishwa na

mwanawe aliyekataa kwenda kumjulia hali nduguye Mwelusi gerezani. Baadaye, habari zinafika kwamba Mwelusi mwenyewe ametoroka. Askari II na Askari III wanafika kwa Tanya, katika harakati za kumtafuta. Gege mwenyewe anadhihirisha ubinafsi. Anapomwuliza mamake kuhusu majilio ya Askari II na Askari III. Tanya mwenyewe anamjibu, *Ungewauliza* (uk.85). Jibu lenyewe linaashiria hasira za Tanya. Kwa hivyo, Gege anashangazwa na matamshi ya mamake. Anamwambia, *Usiendelee kunikasirikia, mama!* (uk.85)

### 3.1.6 Mwanamke kama mtu anayedanganyika kwa haraka

Mwanamke pia anasawiriwa kama mtu anayedanganyika kwa urahisi. Anakosa kudadisi na kutathmini mambo kabla ya kuchukua hatua. Mwandishi anadhihirisha namna ambavyo mwanamke anaweza kudanganyika kwa haraka. Tunamwona Tanya akidanganyika kwa urahisi wakati Gege anapomwendea. Gege mwenyewe anamwelezea mamake kuwa amebadili nia na ameamua kushirikiana na Mwelusi. Ingawa Gege mwenyewe anamhadaa mamake, mama anashindwa kutambua hadaa zenyewe. Moja kwa moja, Tanya anaamini wongo huu wa Gege na kumweleza kuhusu alikoenda Mwelusi. Kwa sababu hiyo, Tanya anafurahi na kusema kuwa *Leo ni siku njema kwangu* (uk 86).

## 3.2 Nafasi chanya na ya kimapinduzi ya mwanamke

Licha ya kubainisha nafasi chukivu anamowekwa mwanamke katika jamii yenye mfumo unaompendelea mwanamume, mwandishi pia ameweza kuangazia nguvu na nafasi chanya anayostahili kupewa mwanamke katika jamii. Amemjenga mwanamke na kuonyesha mchango wake muhimu katika jamii. Mwandishi huyu anadokeza nafasi

muhimu anayostahili apewe mwanamke katika jamii. Anajaribu kuihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kumpa mwanamke hadhi ‘sawa’ na mwanamume. Anaonekana akipigania usawa wa kijinsia kwa kumshirikisha mwanamke katika kuleta mabadiliko ya kiutawala. Mwanamke ana nafasi ya kuchangia katika asasi mbalimbali za kijamii na hivyo, anastahili aachwe ili awajibikie nafasi hiyo vilivyo.Katika sehemu hii, hivyo basi, tumeangazia nafasi yenyewe chanya na ya kimapinduzi anayopewa mwanamke katika *Kifo Kisimani*.

### 3.2.1 Mwanamke kama mtu mwenye bidii.

Mwanamke katika jamii huwa na shughuli nyingi anazotarajiwa kuwajibikia. Kazi zenyewe ni pamoja na kuwalea watoto na kazi za nyumbani. Isitoshe, ana majukumu ya kijamii. Mwandishi amedhihirisha namna ambavyo mwanamke anaweza kujibidiisha na kuwajibikia nafasi yake. Kwa kutumia wahusika wanne wanawake, mwandishi amebainisha nafasi hii muhimu. Hawa ni Kaloo, Tanya, Nyalwe na mamake Atega.

Kaloo akiwa na wanawake wengine wanajibidiisha kuandaa matumbuizo kwa ajili ya mkutano wa Mtemi. Isitoshe anahakikisha amefika uwanjani mapema ili kuandaa uwanja wenyewe vizuri. Katika mazungumzo yake na Mwelusi anamwambia kuwa ameingia mapema kwa ajili ya maandalizi yenyewe (uk 1). Licha ya hayo, anajibidiisha kuhakikisha kuwa mwanawe ameajiriwa. Kushughulika kwenyewe kumefikia kiwango cha  Mtemi kuamuru mwanawe apewe kazi. Hivyo, tunamwona akimwendea Zigu baadaye, ili kutoa shukrani kwa hisani yenyewe. Haya yote yanatokana na bidii za mwanamke Kaloo.

Tanya naye anajibidiisha katika kuwashughulikia wanawe kimalezi. Bidii zake zinamwezesha kuwashughulikia wanawe vilivyo. Mwandishi anatuchorea picha ya mwanamke anayejibidiisha vilivyo katika malezi ya wanawe. Haya yanabainika na namna anavyowashughulikia wanawe: Mwelusi, Andua na Gege. Mwelusi anaposhikwa na 'watu wa Bokono' mamake (Tanya) anasononeka na kukosa utulivu. Akawa anahakikisha mwanawe anapata chakula. Hivyo, akawa anamwandalia chakula na kumpelekea. Wakati mwingine akawa anamtuma Andua. Katika mazungumzo yake na Azena, anasema,

> *Mtoto bado yumo gerezani nimejaribu*
> *kuonana naye, lakini haijawezekana.*
> *Kila mara ombi langu hukataliwa*
> *na Askari wanaolinda gereza. Askari*
> *hawana moyo, wana mawe kifuani.*
> (uk.51)

Uchungu wa mwana unamlazimu kumwandalia chakula na kumpelekea. Nia yake imekuwa ni kumpatia chakula na angalau kuonana naye. Tanya mwenyewe anajaribu kujenga moyo wa udugu na mlahaka mwema baina ya wanawe Gege na Mwelusi. Kwa hivyo, baada ya Mwelusi kushikwa na 'watu wa Mtemi Bokono', anamrai Gege aende akamwone nduguye. Gege anapotoa udhuru, Tanya anakasirika na kumdadisi Gege,

*Anayejaribu kuyawekea*

*maisha yake msingi mzuri*

*hatilii maanani maisha ya ndugu*

*yake?* (uk.43).

Ombi la mzazi huwa ni kuona wanawe wanaishi kwa ushirikiano na mlahaka mwema. Hivyo ndivyo anavyotamani Tanya. Si ajabu hivyo basi, akawa mwepesi kudanganyika kwa kukubali maelezo yake Gege baadaye. Bila kumakinikia mkondo wenyewe, anakubali kauli yake Gege kuwa ameghairi na kuamua kushirikiana na nduguye Mwelusi. Kwa hivyo, moja kwa moja anamshukuru Gege na kumwelezea alikoelekea Mwelusi. Anakiri kuwa, *leo ni siku njema kwangu* (uk.86).

Licha ya hayo, anajitahidi kuwapa wanawe ushauri. Andua anapofika kutoka kisimani, Tanya anashtuliwa na jeraha alilokuwa nalo usoni. Anamdadisi kuhusu hatari ya kutofuata mawaidha: kutembea haraka (uk.49) na kupigana na wenzake. Maelezo yenyewe yanaonyesha na kumbainisha Tanya kuwa mzazi anayewajibika kimalezi. Analishughulikia jeraha lenyewe kwa dharura (uk.49).Yote haya yanamdhihirisha mwanamke huyu kuwa mtu mwenye bidii. Zaidi ya haya, anawajibika kuchukua nafasi anayostahili katika jamii.

Nyalwe ni mwanamke mwingine anayejibidiisha kwa kuhakikisha ameishughulikia familia yake. Anajasiria kumpa ushauri na tahadhari mumewe Bokono kama hatua mojawapo ya kutetea nafasi yake kama mke. Anafahamu kuwa maisha ya ndoa ni ya

watu wawili, mke na mume. Kwa hivyo, anajitahidi kutekeleza wajibu wake katika kumwadilisha mumewe kuhusu uongozi wake. Anajaribu kwa kila njia kumrekebisha mumewe ili azidi kuiongoza Butangi kwa haki. Kwa hivyo, anamwonya dhidi ya washauri wake na kumshauri abadilishe mienendo yake inayowachukiza Wanabutangi. Licha ya hayo, anapanga kuwatembelea wanawe na kuwa nao kwa siku kadha huko Macheleni (uk.90). Huku ni kuwajibika kunakodhihirisha bidii na hivyo, kumdhihirisha kuwa mlezi mwenye bidii. Licha ya hayo, anajitahidi kudumisha ndoa yake kwa 'kumwadhibu' mwanamke yule aliyetuhumiwa kuwa hawara wa mumewe Mtemi (kh.j). Nyalwe pia anajibidiisha kudumisha ndoa yake na Mtemi. Anasabilia kumshauri mumewe kuhusu umuhimu wa kufaana katika ndoa.

Isitoshe, mwandishi ameongeza idadi ya wanawake wanaodhihirisha kuwa na bidii kupitia mazungumzo ya Atega na Kaloo. Kaloo anapomuuliza Atega kumhusu mamake, anaambiwa kuwa amemaliza kupura mbaazi. Kaloo hashangazwi na habari hizi kwani anasema, *Si ajabu, Ni mtu mwenye bidii* (uk.4).

**3.2.2 Mwanamke kama mtu mwenye mapenzi ya dhati.**

Kithaka wa Mberia pia amefaulu kumsawiri mwanamke anayedhihirika kama mtu mwenye mapenzi ya dhati. Katika kubainisha nafasi hii, mwandishi huyu amemtumia mhusika mmoja mwanamke, Nyalwe.

Simone de Beauvoir (1949:652) anaelezea namna upendo au mapenzi yanavyochukuliwa na mwanamke tofauti na mwanaume walioana. Mwandishi huyu anadai kuwa mke katika

ndoa hujisahau na kuendeleza mapenzi ya dhati. Mapenzi ya mwanamke ni ya kihisia na kimawazo, tofauti na mwanamume anayeweza kubadilika baada ya muda. Anasema kuwa ni rahisi kwa mwanamume kubadilika na kumpenda mwanamke mwingine. Kwa mwanamke, mapenzi yake hudumu. Katika tamthilia hii, Kithaka wa Mberia amemwumba mwanamke anayedhihirisha hali kama hii. Huyu ni mhusika Nyalwe. Nyalwe anabainika kuwa na mapenzi ya dhati kwa mumewe na hivyo, anamshughulikia mumewe kwa kila hali. Namna anavyomchukulia mumewe wanapoelekea sebuleni inadhihirisha mapenzi yake kwa mumewe. Anamshika mkono na kumvuta taratibu ili waende kwa maankuli.

Licha ya hayo, amefuatilia mabadiliko anayoyaona kwa na mumewe kwa muda. Kwa mapenzi ya dhati, anamzindua kuhusu wajibu wao yaani mume na mke katika ndoa. Kwamba, wanafaa kuitunza na kuidumisha ndoa yao kwa ushirikiano. Anamwambia Bokono,

> *Ikiwa kuna jambo linalokusumbua,*
> *nieleze. Likiwa zito tulibebe pamoja*
> *Huko ndiko kuishi kama mke Na*
> *mume. Hiyo ndiyo maana ya ndoa.*
> *Kusaidiana kubeba uzito wa maisha.*
> *Kushirikiana katika kupanda miinuko*
> *na kuteremka mabonde* (uk.13).

Baadaye siku hiyo, mumewe anapopiga mayowe na kudai kuwa kaumwa na bafe, Nyalwe kwa mapenzi ya dhati, anamshughulikia kwa dharura. Anaazimia kumwita mganga. Hajui kuwa huo ulikuwa 'mchezo' wa Bokono. Tayari amemshauri kuhusu hatari ya kuwa na wasiwasi. Anagundua wasiwasi wenyewe umesababishwa na uongozi wake mbaya. Kwa hivyo, kwa mapenzi anamshauri mumewe aibadili mienendo inayowaghadhabisha Wanabutangi. Anagundua wasiwasi wake ni hofu ya kupokonywa uongozi. Ingawa anapuuziliwa mbali, anajikakamua kumshughulikia vizuri. Isitoshe, tunaelezwa kuwa, anamwendea katika Ukumbi wa Utawala wa Butangi na kumtahadharisha dhidi ya waandamanaji. Anamwambia mumewe**,** *Tuondoke haraka! Tuondoke kabla hawajafika* (uk.101). Haya yote yanamdhihirisha mwanamke huyu kuwa mtu mwenye mapenzi ya dhati. Ingawa anamshughulikia mwanamume asiyetambua mapenzi yake, anamwonyesha mapenzi halisi.

### 3.2.3 Mwanamke kama mtu mwerevu na mwenye akili tambuzi.

Mwandishi huyu pia amebainisha nafasi chanya ya mwanamke katika jamii. Kwake, mwanamke ni mtu mwerevu mwenye akili tambuzi. Kutokana na yale anayoyasema, na anayoyafanya; mwanamke anaonyeshwa kuwa mwerevu. Wahusika anaowatumia kubainisha nafasi hii ni wanne: Nyalwe**,** Tanya, Atega na Azena. Mhusika Nyalwe anasawiriwa kuwa mwerevu kwa namna tofauti. Kwanza, werevu wake unamfanya apiganie nafasi yake kama mke katika ndoa. Anajua kuwa ndoa ni asasi inayostahili kutunzwa na kudumishwa. Hivyo, anamwelekeza mumewe kuhusu njia za kuidumisha (khj).Anapopata fununu kuhusu uhusiano wa mumewe na mwanamke mwingine, anaamua kumwadhibu mwanamke anayejaribu kusambaratisha ndoa yenyewe (uk. 77).

Pili, anatambua kinachomtia wasiwasi mumewe, kwamba ni wasiwasi wa kupokonywa uongozi. Kwa hivyo, anamweleza hatari ya kuwa na wasiwasi na kumshauri aibadili mienendo yake. Ananasibisha wasiwasi huo, ndoto ya Mtemi na mienendo ya Mtemi Bokono. Huu ni werevu unaomsaidia 'kumtibu' mumewe. Anatambua kuwa, ndoto yenyewe ni picha ya yaliyomo akilini. Na kwamba, Mtemi ana wasiwasi wa kupokonywa uongozi. Pia, anatambua kinachosababisha yote hayo.

Licha ya hayo, anasawiriwa na mwandishi kuwa mtu mwerevu. Anafahamu masuala ya uongozi. Kwamba, watumishi wa umma wanaposhindwa kuwajibikia kazi zao kwa wanajamii, ni kiongozi anayetarajiwa kuwajibika au hata kuwawajibisha kwa kuwatolea amri (uk.19). Kwa kutambua hivyo, anamtanabaisha mumewe Mtemi Bokono aweze kuwajibikia wadhifa wake kama kiongozi wa Butangi. Anamkumbusha kuwa ni yeye anayestahili kunyoosha mambo yanayozua mtafaruku katika jamii ya Butangi. Kwa kumzindua mumewe hivyo, anadhihirisha ana hekima.

Azena na Tanya nao wanasawiriwa kuwa wahusika werevu. Tanya anapotembelewa na Batu kwa ujanja, anagundua ujanja wenyewe. Namna anavyompokea na kumsemea Batu, zinabainisha hekima ya Tanya. Tanya anamwuliza Batu, *Urafiki baina ya kozi na njiwa si kioja?* (uk.76). Baadaye, Batu anapomfafanulia Tanya namna ilivyo 'hatari' kwa Mwelusi kuwa nje ya gereza. Kwamba, *Anaweza kuadhibiwa na wazalendo wa Butangi*.(uk 78) Ujanja huu wote wa Batu haumpigi mshipa Tanya. Kwa hivyo, hayuko tayari kushirikiana na 'Kozi' kwa vyovyote vile. Huu ni werevu anaodhihirisha. Naye Azena anapofika, anawaeleza wote wawili kilichowasibu katika mashambulizi. Batu

anajaribu kutumia fursa hii kumjenga Mtemi Bokono kwa kueleza namna uongozi wake utakavyokabiliana na waliohusika. Tanya na Azena wanamkejeli kwa kauli hiyo. Azena anasema,

*…. bila shaka hatutajali.*
*Kwa nini tujali? Watu kadhaa*
*Wamejeruhiwa. Watu wameuliwa.*
*Mali zetu nyingi zimeharibiwa.*
*Ni binadamu gani wanaojali wakiwa*
*na maisha mazuri kadri hiyo?* (uk.79)

Batu anapoondoka, mazungumzo baina ya Tanya na Azena yanabainisha werevu na uelewa wao wa mambo. Wanajadili kwa mapana kuhusu mashambulizi yaliyowakumba akina Azena na wanakijiji wenzake. Tanya mwenyewe anamfafanulia Azena kuhusu habari zenyewe, namna watu wengine walivyochukulia. Anamweleza kwamba, *Kuna watu wanaosema mashambulizi hayakufanywa na majirani* (uk.81*).* Kwa maoni yake, hiyo ilikuwa ni mbinu ya utawala ya kuwatia woga watu ili waendelee kumsifu kiongozi dhalimu Mtemi Bokono. Huu ni uelewa unaowafanya kuchimbua na kuchanganua hali na mkondo wa mambo katika jamii ya Butangi. Werevu wao unawaepushia hali ya kuendelea kumsifu kiongozi anayezidi kuwanyanyasa wanajamii. Kwao, huu ni uongozi unaostahili kupindusliwa kwa vyovyote vile. Kwa hivyo, wanashirikiana na wazalendo wengine kuupinga utawala wenyewe.

Wote wawili wamefuatilia kwa makini namna uongozi huu umekuwa ukiwatesa na kuwadhulumu wanajamii. Kwa maoni yao, udhalimu katika jamii ulikuwa umefikia kiwango cha kukasirisha. Jamii yenyewe ilikuwa imemkweza kiongozi wao kupita kiwango cha binadamu wa kawaida.  Wanasema Mtemi Bokono alikuwa ameinuliwa hadi kiwango cha kiungu. Azena anasema, *karibu zaidi na Mungu kuliko na binadamu wenzake* (uk.82). Tathmini zao zinawabainisha kuwa werevu na kwamba, wanatambua umuhimu wa kufanya mabadiliko katika uongozi wenyewe. Wanaelewa kuwa baadhi ya Wanabutangi wamezinduka na hivyo, nyimbo za kumsifu kiongozi zilizokuwa zimekita mzizi awali zimefifia. Atega anayechangia katika mjadala wenyewe, anasikitishwa na Wanabutangi wengine ambao bado hawajazinduka. Anaona kuwa ni jambo la kuvunja moyo kuona kuwa baadhi ya wanajamii hadi wakati huu, hawajazinduka na kutambua hali dhalimu waliyomo.

Mwanamke mwingine anayetumiwa na mwandishi kubainisha nafasi hii ni Atega. Mwandishi amemsawiri mwanamke akionyesha ujasiri mkubwa. Atega amewachunguza baadhi ya askari wa Butangi na kutambua kuwa walafi wasiokuwa na uwajibikaji. Kwa hivyo, anaamua kuwategea kitendawili. Tunamwona akiwaletea mkate wa wishwa (wenye tupa ndani) na tembo. Ujanja huu uliorutubishwa na ujasiri unafaulu kumtorosha Mwelusi.  Askari III anapoona tembo ya mfungwa, anashangaa namna marafiki zake mfungwa walivyo na ubaradhuli kama Mwelusi (uk 56). Bila kuukagua mkate wa wishwa, anampa mwenzake Askari II ampelekee mfungwa baada ya Askari I kukataa kuupeleka. Kumbe ilikuwa imepangwa ikapangika njia ya kumtorosha Mwelusi. Kwamba angeletewa mkate wa wishwa ulio na umbo baya pamoja na tembo kwa sababu

askari hao hawangekagua vyakula vyenyewe. Badala yake wangekimbilia tembo kwa sababu ya ulafi wao.

Licha ya haya, ujanja na ujasiri wa Atega unamwezesha kushirikiana na Mwelusi kuwazindua Wanabutangi kupigania haki zao. Ndipo tunamwona akiongea yeye, Tanya na Azena, anasikitisha na baadhi ya wanabutangi ambao hawajazinduka na kutambua hali yao dhalimu. Werevu huu unamwezesha kutathmini huduma wanazopewa Wanabutangi na haki wanazonyimwa. Anaamua kushirikiana na mzalendo Mwelusi. Wote kwa pamoja wanashirikiana kuwazindua wanajamii na hatimaye, kuuangusha utawala dhalimu wa Mtemi Bokono.

### 3.2.4 Mwanawake kama mzalendo jasiri.

Zaidi ya kumwasilisha na kumbainisha mwanamke kama mtu mwerevu, mwandishi ameweza pia kubainisha nafasi chanya ya mwanamke katika jamii. Kwamba, mwanamke ni mzalendo ambaye anajasiria kujitoa kafara kwa ajili ya jamii. Hili ni jambo analodhihirisha. Katika kubainisha nafasi hii, mwandishi amewatumia wahusika wanawake watano: Nyalwe, Tanya, Andua, Atega na Azena. Amewatumia hawa kubainisha nafasi hii katika mazingira tofautitofauti.

Nyalwe anadhihirisha ujasiri wake anapozungumza na mumewe Mtemi Bokono. Huyu ni mwanamke anayejitokeza kama mtetezi wa wanyonge na jamii. Anadhihirisha uzalendo halisi. Anamkabili Mtemi na kumtahadharisha aibadili mienendo yake (uk.15). Anamzindua Mtemi kuwahusu washauri wake wanafiki wanaomdanganya.

Anamwambia**,** *Unadanganywa. Unadanganywa na wanafiki unaowaita washauri waaminifu* (uk.16). Huu ni ujasiri hasa ikizingatiwa kuwa anayeambiwa maneno yenyewe ni Mtemi, mwenye taasubi ya kiume.

Bokono anapopiga unyende, Nyalwe anajasiria kumtobolea siri kuhusu kudorora kwake kiakili. Anamwambia, *Ni kama umri wako unashuka, badala ya kupanda.* (uk.17). Kuhusu mapuuza ya viongozi, Nyalwe anajasiri kumkabili Mtemi Bokono na kumkumbusha kuwa kuwa wanayofanya katika uongozi wao ni kinyume na matarajio ya wanajamii. Nyalwe anaona kuwa mumewe hajawajibikia nafasi yake vilivyo. Bokono anapojigamba kuhusu ujuzi wake wa kanuni, Nyalwe anamwambia,

> *Nakubaliana nawe ! Unazijua*
> *vizuri sana kanuni za ardhi. Na*
> *hapo ndipo pana matatizo. Unazijua*
> *vyema lakini wakati huo huo*
> *unazipuuza kama kwamba huzijui,*
> *kama kwamba hazipo!* (uk 19).

Anamtahadharisha dhidi ya washauri wake wanafiki na mabarakala. Picha tunayopata ni ya mzalendo halisi asiyefurahia dhuluma dhidi ya wanajamii wengine. Anamtetea Mama Agoro anayefika kwake ili kuwasilisha malalamiko kwa Mtemi. Mama Agoro ametumwa kuwasilisha malalamiko kuhusu kunyakuliwa kwa uwanja wa kuchezea watoto wao (uk.19).

Tanya naye anajasiri kuupinga uongozi dhalimu wa Mtemi Bokono. Anapomwaga dukuduku lake mbele ya Batu, anamwambia, *Sijamwona tangu akamatwe na watu wa Bokono* (uk.78). Anasema hivyo kumjibu Batu kama amemwona mwanawe Mwelusi. Batu alikuwa katika harakati za kumtafuta Mwelusi aliyekuwa ametoroka gerezani. Anasema na Batu kwa ujasiri mwingi. Huyu ni mshauri wa Mtemi Bokono na ni mtu anayeendeleza taasubi ya kiume. Lakini yote haya hayamzuii Tanya kuonyesha kuudhika kwake na uongozi dhalimu. Kwa Tanya, askari wanaofaa kuwahudumia Wanabutangi wanamhudumia kiongozi na watu wake tu.

Andua naye anajikakamua na kuupinga uongozi huu dhalimu wa Mtemi Bokono. Anapotumwa na mamake ampelekee Mwelusi chakula, Andua anatii maagizo ya mamake na kuelekea gerezani. Anapofika, anajasiri kuwazungumzia askari kwa ujasiri mwingi. Haja yake ni kutimiza maagizo ya mamake. Anamsisitizia Askari III kwamba, yeye mwenyewe (Andua) atampa chakula Mwelusi kama alivyoelelekezwa na mamao.(uk 35). Anapotishwa na Askari III huyu, kuwa angezabwa Kofi, anamwuliza, *Kwa nini? Kwa nini nipigwe kofi?* (uk.35) Awali, Andua mwenyewe alikuwa anadhihirisha ujasiri kutokana na yaliyomsibu kisimani. Mwandishi anazidi kutusawiria mtu jasiri. Anapoingia nyumbani na jeraha usoni, mamake anamdadisi. Naye anaeleza namna yeye na wateka maji wengine walivyojasiria kuchota maji. Walivunja kanuni kwa ujasiri na kuelekea Kisima cha Mkuyuni. Siku hiyo hawakuwa wanaruhusiwa kuteka maji. Lakini wanawake wenyewe wakaamua kwenda kisima hicho. Kwa hivyo, kulingana na maelezo anyotoa Andua, hatua yao ya kuvunja kanuni ilimfanya ajeruhiwe.

Hatua hii inamwonyesha Andua kuwa mwanamke jasiri. Kutokana na maelezo ya Tanya, bado Andua yuko tayari kuelekea kisimani.Baada ya Mwelusi kutoroka gerezani, Mwelusi na Atega wanafika nyumbani na kuulizia alikokuwa Andua. Tanya anaeleza kuwa Andua mwenyewe ameelekea Kisima cha Mkomani (Kilichopigwa marufuku).Mama anasema *Yeye pia amekuwa* jasiri. *Ana habari kamili. Lakinialisema badoatajaribu kuteka maji* (uk.83*).* Anapofika kisimani siku hiyo, anajibizana na Zigu kwa ujasiri mwingi. Anadadisi uongozi wa  Mtemi Bokono uliojaa udhalimu. Kwa Andua, Mtemi Bokono anatumia Baraza la Wazee, kanuni na Baraza la Hukumu kuendeleza na kudumisha uongozi wake dhalimu. Kwake uongozi huu unaelekea ‘kuondoa uhai wa umma kutoka kwa umma’ kwa kukataza watu kuteka maji. Picha inayojitokeza ni ya mzalendo jasiri anayeuhoji uongozi dhalimu. Amejikomboa kiakili na anajua haki zake kama Mwanabutangi. Anamwambia Zigu,

> *Haki ya mwanabutangi juu ya*
>
> *Butangi. Nina haki ya kutumia*
>
> *maji ya Butangi.* (uk.92)

Ujasiri huu wa kizalendo ndio   unaostahili kukuzwa na kutunzwa. Kwa hivyo, mwandishi amewaumba wahusika wanawake majasiri kama mchango wake katika kuwahamasisha wanajamii kuhusu haja ya kutambua na kukuza nafasi na utambulisho wa wanawake. Anahakikisha majasiri wenyewe hatimaye, wanafaulu kuupindua uongozi huu mbaya wa Mtemi Bokono.

Atega anasawiriwa na mwandishi kama mzalendo jasiri tangu mwanzo wa tamthilia. Anaukabili uongozi vilivyo. Anashirikiana na mzalendo mwenzake Mwelusi katika kuwazindua wanajamii. Kaloo anapomwuliza kuhusu urafiki wake na Mwelusi, anasema kuwa unatokana na masuala ya Butangi (uk.5). Mwelusi anapofungwa, anazua mbinu ya kumtorosha ili waweze kuendeleza harakati za ukombozi wa Butangi. Nia yao ni kuwa jamii ipate kuongozwa vyema. Baada ya kushirikiana na wengine kumtorosha Mwelusi, yeye Mwelusi wanaendeleza harakati za kuikomboa jamii ya Butangi. Yeye na Mwelusi wanapokwenda kisiman wanampata Zigu pale. Pale kisimani, anamzindua Zigu kuwa,

> *Na kukomboa kisima na Bonde*
> *la Ilangi hakutakuwa mwisho*
> *wa safari yetu. Leo ni siku ya*
> *kuanzisha Butangi mpya*.(uk.94

### *3.3 Hitimisho*

Sura hii imechunguza nafasi na utambulisho mwanamke katikatamthilia *Kifo Kisimani*. Msanii amefaulu kubainisha nafasi hasi anayopewa mwanamke katika jamii inayomkweza na kumwenzi mwanamume. Tumefafanua namna ambavyo mwandishi mwenyewe amebainisha nafasi dhalilishi na dunishi anayopewa mwanamke na kwamba, baadhi ya wanajamii humchukulia mwanamke kuwa chombo cha kumfurahisha mwanamume,mtu mwenye umbeya, barakala anayejipendekeza kwa viongozi ili afaidi, kiumbe duni awezaye kufanyiwa chochote, mwongo, mwingi wa hasira na fisadi. Kwa kutumia wahusika mbalimbali (wanawake kwa wanaume), mwandishi anafaulu kubainisha nafasi hii chukivu inayopewa mwanamke. Na kwa kiasi fulani baadhi ya

wanawake wenyewe wanaonekana kuridhika na nafasi yenyewe. Hata hivyo, anadhihirisha baadhi ya wanawake wasioridhika na nafasi yenyewe.

Anadhihirisha nafasi chanya anayostahili kupewa mwanamke katika jamii. Kwamba, mwanamke ni mwanajamii anayeweza kujibidiisha vilivyo katika ujenzi wa jamii mpya, mwenye mapenzi ya dhati, mwerevu na mwenye akili tambuzi, mzalendo jasiri na mlezi mwema.

Kwa hivyo, mwandishi Kithaka wa Mberia amefaulu kubainisha nafasi chanya na utambulisho wa mwanamke katika jamii. Anabainisha hayo katika *Kifo kisimani* kama tulivyoonyesha katika sura hii.

# SURA YA NNE

## CHANGAMOTO ZINAZOKABILI HARAKATI ZA KUMKOMBOA MWANAMKE.

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeangazia changamoto zinazokabili harakati za kujenga usawa wa jinsia katika jamii. Kwa muda sasa, harakati zenyewe zimeendelezwa na wataalamu wa ufeministi na hasa wanawake. Hata hivyo, kama inavyodhihirika katika *Natala* (1997) na *Kifo Kisimani* (2001), bado kuna changamoto kadha. Tumezibainisha changamoto zenyewe kwa kuziweka katika makundi manne: asasi za kitamaduni, hali ya kutojua miongoni mwa wanawake, masuala ya kiuchumi na ukosefu wa ushirikiano kati ya wanawake wenyewe.

### 4.1 Asasi za Kitamaduni

Kila jamii ina utamaduni unaowaelekeza na kuwaongoza wanajamii na maisha yao. Asasi za kitamaduni zinaonekana kuwa zimejengeka kwa namna inayompendelea mwanamume na kumdunisha mwanamke. Wakigusia suala lenyewe, Wanjiku na Akinyi (1993:69), wanadadisi mtazamo hasi unaobainika wazi dhidi ya mwanamke. Wanahoji kwamba, utamaduni aghalabu humkweza mwanamume na kumtweza mwanamke. Nao Pilcher na Imelda (2004:65), wanasema kuwa kuna ithibati tosha kuonyesha ugavi wa majukumu kulingana na jinsia ya mwanajamii. Wanathibitisha madai yao kwa kurejelea mawazo ya Hartman (1982). Hartman anaeleza hali ambapo jamii inawagawia wanajamii majukumu kwa kufuata utaratibu maalum. Kazi za staha zinfanywa na wanaume. Zile

zinazoonekana kuwa 'duni' zinaachiwa wanawake. Wanaona kuwa huu ni ubepari wa kijinsia: Kulingana nao, jamii yenye mfumo kama huu huendeleza utabaka wa kijinsia. Hartman, kwa mujibu wao anaelezea namna wanaume hufaulu kudumisha hadhi yao ya juu. Anaona ukuruba baina ya ubabe-dume na ubepari. Kutokana na hali hii, mwanamke hugawiwa majukumu mengi ya kinyumbani.

Katika *Natala* (1997), mhusika mkuu anatumiwa na mwandishi kudhihirisha hali hii. Mhusika mwenyewe anajibidiisha katika kazi za nyumbani. Mumewe yuko mjini Ruma- Tangu mwanzo wa tamthilia yenyewe, Natalala anashughulikia kazi za nyumbani: kuvua nguo, kuzipiga pasi na kuwalea wanawe. Tila naye anaingia kwa Natala kwa ajili ya kuomba chumvi. Awali, alikuwa amejia sukari na mafuta ya taa. Zote hizi zinadhihirisha shuguli zinazohusika ni za nyumbani. Utamaduni umemwajibisha mwanamke katika shughuli za nyumbani.

Katika *Kifo Kisimani* (2001), wanawake wanawajibikia kazi za nyumbani. Andua anaelekea kisimani kuteka maji na hivyo kukabiliana kijasiri na Zigu (khj). Pia, anamsaidia mama kumpelekea nduguye chakula gerezani. Atega na Tanya wanandaa vyakula na kumplekea Mwelusi gerezani. Licha ya hayo, Tanya anashughulikia malezi ya wanawe, anadondoa nafaka na mapishi. Katika mazungumzo baina ya Kaloo na Atega, Kaloo anauliza kuhusu mamaye Atega. Anauliza kama amemaliza kupura mbaazi.

Shughuli hizi zote zinabainisha majukumu ya mwanamke kitamaduni. Anawajibikia kazi za nyumbani na malezi ya watoto. Hata hivyo, shughuli hizi zote zinakosa kumfaa

mwanamke kiuchumi. Majukumu yenyewe yanakosa kutambuliwa na kuthaminiwa na jamii. Kulingana na ripoti kuwahusu Wanawake Ulimwenguni (1985:13), inabainika kuwa asilimia 40 za familia nchini Kenya, Botswana, Ghana na Sierra Leone zinasimamiwa na wanawake. Wanawake wenyewe wanafanya kazi nyingi hasa za kilimo na malezi. Hata hivyo, ripoti yenyewe inaeleza namna mchango huu unakosa kutambuliwa na kuthaminiwa na jamii. Hii ina maana kuwa mwanamke huwajibika siku nzima lakini hukosa kupiga hatua kiuchumi. Katika kuthibitisha hali yenyewe, Fredrik Schjander alifanya utafiti nchini Tanzania *(We women,* 1952:2) na alipomhoji mwanamke mmoja (Hadija Muyombo) aliyethibitisha ukweli huu. Mhoji anatoa picha halisi ya nchini Tanzania, ambapo mwanamke anatarajiwa kufanya mengi. Mhojiwa mwenyewe alithibitisha kuwa jamii huwawajibisha wanawake na hata wasichana. Anasema kuwa mvulana huwa hapewi majukumu mengi. Wanawake na wasichana wanatarajiwa kunadhifisha nyumba, kuandaa chakula, kuchota maji na kazi nyingine za nyumbani. Kwa upande mwingine, mvulana hutarajiwa kuwachunga mifugo tu. Kithaka wa Mberia amedhihirisha hali yenyewe katika *Kifo Kisimani*. Gege anajishughulisha na masuala ya kibinafsi, kutengeneza ala ya muziki. Naye Andua anamsaidia mamake Tanya katika shughuli za nyumbani. Anaenda kisimani kuchoka maji, anamsaidia mamaye kumpelekea nduguye Mwelusi chakula gerezani.

Kwa sababu ya nafasi chukivu anayopewa mwanamke kutokana na mfumo wa kitamaduni, baadhi ya wanawake wanaudhika. Katika *Utengano* (1980:7), mhusika Kazija ananung'unika na kumwaga dukuduku lake. Anaelezea machukizo yake kwa mwanamke na jamii. Anadadisi jamii kwa kumwekweza mwanamume na kumdhalilisha

mwanamke. Asasi za kitamaduni zinazodhirika kukwamiza na kuzikabili kiukinzani harakati za ukombozi ni; hali ya kutamani tofauti, asasi ya ndoa na kutoshirikishwa kwa mwanamke katika maamuzi.

### 4.1.1 Asasi ya Ndoa

Kila mwanajamii hutamani kuheshimiwa, kusikilizwa na kupewa haki yake. Sawa na mume katika ndoa, mke huhitaji staha na heshima. Hata hivyo, jamii nyingi za Kiafrika humtarajia mwanamke kumheshimu mume na kumnyenyekea. Aghalabu, nafasi anayopewa mke ni duni, chini ya mume. Kwa sababu hiyo, baadhi ya wake wamerengeka na kukubali hali yao katika ndoa. Huelekezwa na matakwa ya waume zao. Wakielezea hali yenyewe, Nune na Dearma (1972:96) wanadadisi jamii kwa hilo. Wao wanarejelea kitabu cha Greer *The Female Eunuch* (1970) kinachofafanua hali ya mke katika ndoa. Greer mwenyewe anadhihirisha namna harusi inavyomtosa mwanake katika hali chukivu. Anasema hali inayotokea baada ya harusi aghalabu ni ya kutamausha. Humfanya kuwa mtumishi wa nyumbani anayemtegemea mwanamume.

Tuckwell na Moore (1975:2) nao wanasema kuwa wake katika ndoa hulazimika kunyenyekea mbele ya waume zao. Wanasema kuwa wanawake huwa na masuala yanayowahusu na huhitaji kushughulikiwa. Hata hivyo, wanawake wenyewe hulazimika kunyamaza. Hii ni kwa sababu ya kuogopa matokeo ya mjadala kama huo. Wanaeleza kuwa chanzo cha hali hii ni malezi. Mume huandaliwa kimalezi kuwa mdhibiti katika familia. Mke naye kuandaliwa awe na unyenyekevu kwa mumewe. Tuckwell na Moore

wanasema kuwa wake wenyewe huogopa kuchukuliwa kuwa waasi wa utamaduni kwa kupinga utaratibu wa jamii yao.

Hali hii inadhihinishwa na mwandishi Kithaka wa Mberia. Mama Lime anamshauri Natala kuhusu manufaa ya kurithiwa kama mke. Anamwambia Natala, *Kuwemo na zaidi ya mke mmoja nyumbani kunahakikisha kuridhika kwa mume* (uk,39). Na kwamba, kuridhika kwa mume kunaleta ushwari nyumbani (uk. 39). Ni sawa na kumwelekeza kuwa bila kumridhisha mume katika ndoa, ushwari utakuwa haupo. Ni mpaka aridhike ndipo kuwe na ushwari. Ni wake wachache tu wawezao kujasiria kupinga matarajio kama hayo katika jamii. Natala anaonekana kuelewa hali itakayomfika endapo angekubali kuwa mkewe Wakene. Anasema, *Na Nafasi yangu nyumbani ndogo* (Uk. 39). Natala anapinga utumwa kama huu ambapo anapewa ‘nafasi ndogo’.

Nyalwe naye (*Kifo Kisimani)* anajasiria kwenda kinyume na matarajio ya jamii kwake,, na kumkabili mumewe, Mtemi Bokono. Anamshauri mumewe kuhusu suala la ndoa na haja ya kufaana katika ndoa. Licha ya hayo, anamtahadharisha kuhusu uwajibikaji unaoonekana kukosekana katika uongozi wake. Ni wanawake wachache wanaojasiria kuenda kinyume na matarajio utamaduni wa jamii yao. Kukosekana kwa ujasiri kama huu kunadumisha ubabe-dume katika jamii. Greer (1970) anapendekeza suluhu kwa tatizo hili. Kulingana na Wafula na Njogu (2007:90) Greer anawahimiza wanawake wasusie ndoa kwa sababu hali hii huwanyima uhuru wao. Anasema ndoa humfanya mwanamke kumulikiwa na hivyo kukosa maamuzi huru.

### 4.1.3 Uhafidhina

Utamaduni katika jamii aghalabu huongoza maisha ya wanajamii, matarajio yao na hata utendakazi wao kijamii. Kulingana na Pilcher na Imelda (2004:1), wafeminsti wanashuku kuwa uhafidhina ni pingamizi katika uletaji wa usawa wa kijinsia katika jamii. Wanalaumu hali ya kutamani tofauti za kiwajibu kulingana na jinsia katika jamii. Aghalabu, wanawake kwa wanaume wangependa kuwe na mpaka bayana wa kiwajibu kulingana na jinsia. Kwa kuzingatia mtazamo huu, nafasi ya mwanamke huchukuliwa kuwa jikoni na ulezi wa watoto. Aghalabu jamii nyingi hasa za Kiafrika humtarajia mwanamke kuwajibikia kazi za nyumbani na malezi ya watoto. Naye mwanamume hutarajiwa kushughulikia masuala ya ulinzi, uongozi na maamuzi. Mawazo haya ni ya kihifadhiwa kwa hakuna kidumucho isipolkuwa mabadiliko yenyewe. Kwa sababu ya uhafidhina, mwanamke akitekeleza ‘wajibu wa mwanamume’, huchukuliwa kakiuka mipaka. Ni sawa na mwanamume kutekeleza ‘wajibu wa mwanamume’.

Mwandishi Kithaka wa Mberia amedhihirisha hali hii katika *Natala* na *Kifo Kisimani*. Katika *Kifo Kisimani*, Zigu anamwona Andua kakiuka mipaka kwa kuingilia masuala asiyoyajua pale kisimani. Katika udadisi wake kwa Andua kwa kuenda kisimani, Andua anamfafanulia kuwa yeye Zigu anafaa kuheshimu haki yake, Andua. Zigu akawa anaona kuwa Andua anatumia neno haki ilhali haliji. Anamwambia, *Usitumie neon usilolijua. Haki. Haki gani?* (uk.92). Kwake Zigu, haya ni masuala ya uongozi yasiyojulikana kwa mwanamke, hasa msichana mdogo kama Andua. Sawa na Andua, Zena anaonekana kukiuka mipaka kwa kujitosa katika ulingo wa siasa. Katika *Utenzi wa Moyoni* (*Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, 2004), Zena anakabiliwa na pingamizi chungu

nzima. Baadhi ya wanajamii hasa wanawake wanamhukumu na kumdharau. Kwao, wanaona kuwa wanaume wameshindwa kuwaongoza na hivyo mwanamke atawezaje? Wanaamini kuwa kinachomshinda mwanamume, mwanamke hata hafai kujaribu.

Licha ya hayo, jamii humnasibisha mwanamume na uhimili au uthabiti katika familia. Ithibati tosha ya dhana hii ni urithi wa mwanamke katika jamii nyinyi za Kiafrika. Jamii zenyewe humrithisha mwanamke endapo mumewe atafariki. Mke hutafutiwa mhimili mwingine. Utafiti uliofanywa katika jamii za Afrika Magharibi (Women and The Law ni West Africa 2003:179) ulibainisha kuwa wanawake wanazidi kudhalilishwa. Utafiti wenyewe unabainisha kuwa ni jambo la kawaida kwa mke na wanawe kurithiwa. Mke aliyefiwa hurithiwa na mwanamume anayekurubiana na mumewe. Jamii huamini kuwa mke kama huyu atapata kutunzwa na mume huyu anayemrithi. Utafiti wenyewe hata hivyo, unabainisha madhila mengi yanayotokea mume anapoaga dunia: kutotunzwa kwa mke na wanawe, kunyanganywa mali yao na mengine mengi. Kithaka wa Mberia ameibua suala hili la urithi wa mwanamke. Baada ya mumewe ‘kuaga dunia’, Natala anapangiwa na wazee wa ukoo akarithiwe na Wakene. Maamuzi ya wazee wa ukoo yanawasilishwa kwake Natala kupitia Mama Lime. Natala anakataa maamuzi yenyewe na kuamua ‘kupitia njia nyingine’. Kwa sababu ya kukiuka matarajio ya wazee wa ukoo, Natala anakabiliwa na adhabu kali: kutafuta makao mengine mapya, kunyang'anywa cheti cha shamba, lakini watoto wabakie katika familia.

Isitoshe, jamii aghalabu humchukulia mwanamke kuwa kiumbe duni asiyejiweza kijamii. Huhitaji ulinzi na usalama wa mwanamke. Aghalabu, mwanamke ambaye hajaolewa

katika jamii nyingi za Kiafrika hukosewa heshima na kunyanyaswa kimapenzi. Naye mke wa mtu hupewa heshima na staha hasa akiandamana na mumewe (*Re-thinking Sexuality in Africa*, 2004:163). Machera anafafanua baadhi ya masuala nyeti yanayohusu mambo ya uana. Anasema kuwa wanafunzi wake chuoni humhoji kuhusu hali dhalimu wanaopitia wanawake 'wasio na waume' kwamba hukosewa heshima katika jamii. Machera mwenyewe anasema kuwa wanawake wenyewe aghalabu huchukuliwa kuwa hawara na kubandikwa majina ya kimatusi. Mwandishi Kithaka wa Mberia ameibua suala lenyewe katika *Natala* (1997) na *Kifo Kisimani* (2001). Katika *Natala*, mhusika Natala anasumbuliwa na mhudumu wa Jengo la Ufuo. Kwa sababu ya kuwa peke yake mle ndani, anasumbuliwa kimapenzi. Hali hii inathibitisha maoni yake Machera kuhusu yanayompata mwanamke katika jamii. Machera anasema kuwa mwanamke aghalabu anakosewa heshima anapotembea paka,bila kuwepo kwa mwanamume. Andua naye (*Kifo Kisimani*, 2001) anasumbuliwa na Askari III kwa kufika gerezani peke yake. Kwa sababu hiyo, anatishwa kwamba angezabwa kofi kwa kujibizana naye. Anapouliza sababu ya kupigwa kofi, anaambiwa kuwa angefanyiwa mengine. Mwandishi anadhihirsha ubabe-dume (Askari III) katika jamii hii. Askari mwenyewe anawaamrisha wanawake (Atega na Tanya) waondoke. Na katika tukio jingine, anamwangusha Tanya. Hii ni baada ya Tanya kukosa kumjulisha walikoelekea Mwelusi na 'Malaya wake'. Askari mwenyewe anampachika Atega jina la matusi, Malaya.

Inayodhihirika ni hali dhalilishi aliyoko mwanamke katika jamii. Uhafidhina huu unaonekana kukwamiza harakati za kumkomboa mwanamke. Kwa hivyo, udumishaji wa

uhafidhina utadumisha ubabe-dume. Hii itamaanisha kuwa mwanamke azidi kuitikia hali dhalilishi na mwanamke kudumisha hadhi yake ya juu.

### 4.1.4 Wanawake kutoshirikishwa katika maamuzi

Maamuzi ya masuala ya kijamii katika jamii nyingi za Kiafrika aghalabu hutekeleziezwa na mwanamume. Jamii zenyewe humpa usukani na udhibiti mwanamume. Kwa hivyo, maamuzi ya familia, jamii na maisha kwa ujumla ni shughuli za mwanamume. Ingawa mwanamke huwa na mchango muhimu katika maamuzi ya masuala ya kijamii, aghalabu hashirikishwi. Wataalamu wa Ufeministi wa tapo la Kiafrika wanahoji kimya cha kulazimishwa katika jamii. Wanasema kuwa mwanamke hulazimika kunyamaza hata pale ambapo mashauriano yangefaa zaidi. Kwa maoni yao, mwanamke katika jamii za Kiafrika hulazimika kuitikia maamuzi ya mwanamume. Jamii zenyewe za Kiafrika huwa na mfumo wa utawala unaongozwa na baraza la wazee. Baraza lenyewe huundwa na wanaume pekee. Mfumo kama huu hautakosa kuendeleza upendeleo katika maamuzi yake. Kwa hivyo, Wanjiku na Akinyi (1993:5) wanahoji hali yenyewe. Wanasema kuwa *maamuzi yaliogozwa na wazee (wanaume) waliofanya maamuzi yanayoihusu jamii, uongozi huu haukumshirikisha mwanamke. Mwanamke hangeonekana uongozini wala kusikika TY*.

Wanarejelea mfumo wa uongozi katika jamii za Wajaluo na Wakuria, nchini Kenya. Mfumo kama huu aghalabu hukosa kutilia maanani vilivyo maslahi ya wanawake. Mhusik Natala *(Natala*, 1997) hashirikishwi katika maamuzi ya kumrithisha. Maamuzi yenyewe yanafanywa na baadaye Mama Lime anatumwa akampelekee maamuzi

yenyewe. Natala mwenyewe anaelewa yatakayomfika kama mke aliyerithiwa. Kwa hivyo anakataa maamuzi yenyewe. Anaadhibiwa kwa sababu ya kukataa (khj).

Waruhiu anatoa mchango wake katika makala yake ya *What Do African Women Want?* (*A Diplomacy of the oppressed: New Direction in International Feminism* 1995:143). Anaibua suala hili linalohusu uongozi. Kwamba wanawake wanakosa kushirikiswha katika masuala ya kijamii hasa maamuzi yao. Kwa maoni yake, hatua hii huchangia kumdidimiza mwanamke katika hali dhalilishi. Hii ni kwa sababu maslahi yao yanakosa kushughulikiwa vilivyo katika smaamuzi yanayonuiwa kushughulikiwa. Clara Momanyi anaibua suala hili katika hadithi yake fupi *Ngome ya Nafsi* (*Mayai Waziri Wa Maradhi and Hadithi Nyingine*, 2004). Hadithi yenyewe inasawiri hali inayomkabili mke katika maamuzi ya kifamilia. Mumewe Bi. Kija anapanga ndoa ya bintiye Naseko bila kumhusisha mkewe. Bi. Kija anashangazwa baada ya kujulishwa na wanawe wadogo. Kwa hivyo, anaamua kujifungia ndani na kulia kwa kufahamu kuwa mwanawe Naseko angeolewa na mwanamume katili, Mzee Sakaja. Hangekubali Naseko aolewe na kikongwe huyo mzee lakini hakushirikiswa katika maamuzi yenyewe.

Katika *Kifo Kisimani (2001)* mwandishi anadhihirisha hali kama hii. Uongozi wa Mtemi Bokono haushirikiashi mwanamke yeyote. Wote ni wanaume: Mtemi, washauri wake, askari na hata makachero. Ripoti ya Umoja wa Mataifa Kuhusu Wanawake (2000:XVI) inatambua haja ya kuwashirikisha wanawake katika maamuzi mbalimbali ya kijamii. Inaaminiwa kuwa hatua yenyewe itachangia katika kujenga usawa, kufikia malengo ya usawa, maendeleo na amani kwa wote. Ripoti yenyewe ilipendekezea serikali

mbalimbali zitekeleze mapendekezo yenyewe. Kulingana na ripoti yenyewe The World Women (2000). Mkutano uliofanyika Beijing mwaka 1995 ulikuwa umependekeza hatua za kuchukuliwa. Hatua zenyewe zingehakikisha wanawake wameshirikiswha kikamilifu katika nyadhifa mbalimbali za uongozi. Hata hivyo ilionekana baadaye kuwa haya hayakutiliwa maanani kufika mwaka 2000. Kwa hivyo ni changamoto inayokabili harakati za ukombozi wa mwanamke, utakaohakikisha kuna usawa wa kijinsia katika jamii.

**4.2 Hali ya kutojua miongoni mwa wanawake wenyewe.**

Hali ya kutojua ni moja miongoni mwa changamoto zinazokabili na kukwamiza harakati za kumkomboa mwanamke kutokana na ubabe-dume. Wanawake wengi wanaonekana kutoelewa haki zao. Kulingana na Biblia Takatifu, watu wengi hupotea kwa sababu ya kukosa ufahamu. Kwa sababu ya hali hii ya kutojua, wanawake wenyewe wanatosheka na hali inayowakumba. Pilcher na Imelda (2004:49) wanaibua suala lenyewe. Wanafafanua mawazo ya wataalamu wa Ufeministi wa Kiharakati wanaolaumu hali ya kutosheka miongoni mwa wanawake. Kwa maoni yao, kutosheka huko ndipo kunakokwamiza ujengaji wa usawa wa kijinsia katika jamii. Wanasema kuwa (2004:41), "*wengi hawataki kufanyia mapinduzi mpangilio wa kihadhi ili wapate angaa kuimarisha hali yao kihadhi.''* TY

Maoni hayo yanaungwa mkono na Wanjiku na Akinyi (1993:1). Wanadadisi hali ya mwanamke katika jamii. Wanapendekeza mwamko wa wanawake ili wajue kuwa

mfumo uliopo katika jamii ulizuliwa na wanajamii, Na kama ulizuliwa, unaweza kubadilishwa ili kuimarisha hali ya mwanamke kijamii.

Hatua ya Mama Lime kukubali kutumwa na wazee wa ukoo kumpelekea ujumbe Natala ni ithibati: mwanamke ameitikia hali yake dhalilishi kiasi cha kuamini kuwa familia bila mwanamume ina shida. Kwa hivyo, mume anapoaga dunia, ni sharti mhimili mwingine atafutwe. Mama Lime mwenyewe anamwambia Natala, *Nija nzuri ya kuwalea bila shaka ni kushirikiana na mwanamume. Unahitaji usaidizi* (uk. 36). Huu ni uhafidhina unaompa mwanamke kutojiamini kujisimamia na kuwa huru kimawazo.

Badala yake humdimiza katika hali gandamizi. Humpa mawazo ya kijidunisha na hivyo kujiona mtegemezi wa kudumu, wa mwanamume. Mama Lime haamini kuwa Natala (mwanamke) aweza kujisimamia bila mume mwingine. Kwa hivyo anampa 'ushauri' afikirie kuhusu kumtafuta mhimili mwingine. Kwa Mama Lime, malezi yssa watoto hauwezi kufaulu bila uwepo wa mume. Wanawake wengi wana mawazo sawa na Mama Lime. Ni wachache tu wanaoweza kukabili na kupinga mawazo ya kihifadhina yanayowadhalilisha.

Katika utafiti uliofanywa katika eneo moja huko Afrika Magharibi, ilibainika kuwa wanawake wengi hawaelewi haki zao. Kulingana na ripoti yenyewe. *Women And Law In West Africa (2003:179)* hali yenyewe imezidi kudumu. Ripoti yenyewe inaeleza kuwepo kwa kanuni katika dini ya Kiislamu zinazompa mwanamke haki ya kurithi mali. Hata hivyo, kwa sababu hana ufahamu wa sheria hizi, anakosa haki yake. Mwandishi

Rayya Timammy naye anadhihirisha hali kama hii katika jamii aliyoitungia hadithi yake fupi *Uteuzi wa Moyoni* (*Mayai Waziri wa Maradhi wa Hadithi Nyingine*, 2004). Zena anapotoa ahadi katika kampeni kuwasaidia wanawake, baadhi ya wanawake hawaoni sababu ya kusaidiwa. Wanatosheka na hali yao. Wanasema, *Shida gani tulizo nazo? Twala, twavaa tuna kasoro gani?* Kwani hata kama hatukwenda skuli ndiyo nini? (uk 16). Mwandishi huyu anawatumia wanawake hawa kuwawakilisha wanawake wengi wa barani Afrika wasiojua haki zao. Wanatosheka na hali yao na hivyo kukwamiza mapambano dhidi ya ubabe-dume katika jamii.

### 4.3 Mfumo wa Kiuchumi

Kikwazo kingine kinachokabili ufanisi wa harakati za kujenga usawa wa kijinsia ni uwezo duni wa mwanamke kiuchumi. Ni mwanajamii anayejiweza na kujitegemea anayeweza kudai haki yake. Hii ni kwa sababu mhitaji hana chaguo isipokuwa kuitika matakwa ya mfadhili wake ilivyo na kwamba, aghalabu wanawake wengi huwa hawajiwezi kiuchumi. Hulazimika kuwa wategemezi wa wanaume kiuchumi. Kwa hivyo, hulazimika kunyenyekea mbele ya waume zao wanapoolewa. Kwa sababu wanaume wanaelewa udhaifu huu wa wanawake, wanajihifadhia hadhi kwa kuwapa wanawake masharti fulani. Natala anajipata katika hali ya mtanzuko kwa sababu ya kutopewa uteuzi: wazee wa ukoo wanamwamulia arithiwe na Wakene, hataki kurithiwa na Wakene na ndipo anapewa maagizo atafute pa kuhamia. Anafanyiwa hivi kwa sababu mfumo wa jamii unamtambua mwanamume kuwa mmilki mali. Kwamba mwenye mali ameaga dunia na hivyo atakayerithi ni nduguye au mwanamume anayekurubiana naye.

Kwa maoni ya Natala, mali waliyojichumia na mumewe Tango Mwine ni yao. Ndipo anamwambia Mama Lime,

> *Sina nia ya kwenda kwingine.*
> *Ninataka papa hapa. Nitaendelea*
> *kuishi katika nyumbahii tuliyoijenga*
> *na mume wangu.Nitaendelea kulima*
> *shamba hili* (Uk. 36).

Mawazo haya ni ya mtu aliyepevuka kiakili. Lakini jamii hautambua mchango wake, Taylor (1985:74) katika makala yake *Women: a World Report (1985:74)* anagusia suala hili. Anaelezea namna mtoro msichana huwasaidia wazazi wake. Punde anapoolewa, anamsaidia mumewe kuchuma mali. Anaeleza hata hivyo kuwa mchango huu wote unakosa kutambuliwa na jamii. Waruhiu (khj) ana maoni kama ya Taylor kuhusu hali ya mwanamke ya kiuchumi. Anasema kuwa mwanamke aghalabu kukosa kupiga hatua kiuchumi kwa sababu ya kutomiliki nyenzo kuu za kiuchumi. Anaangazia suala lenyewe kwa kurejelea bara la Afrika, ambapo umaskini ni suala nyeti. Anaona chanzo cha hali yenyewe kuwa ni kasumba za kikoloni, utamaduni, mifumo ya kisiasa na sera zisizofaa *(What Do African Women Want?* 1995:137).

Mfumo wa kiuchumi humpa mwanamume umiliki wa nyenzo za kuzalisha na kudhibiti mali. Jamii nayo inamwona mwanamke kama msaidizi wa mwanamume lakini hamiliki chochote. Badala yake, anahesabiwa kuwa sehemu ya mali ya mume au mwanamume.

Mke, watoto, shamba na mifugo ni mali ya mwanamume. Akifafanua suala hili, Newland (1979:12) anasema kuwa jamii nyingi zinaonekana kuendeleza ubaguzi wa kijinsia dhidi ya wanawake. Anasema katiba za kisasa zinaonekana kumpendelea mwanamume. Anatoa mfano wa kanuni za Kirumi zilizosanifishwa na Napoleon Benaparte ambazo zinamkweza mwanamume na kumtweza mwanamke.Kanuni zenyewe zinamchukulia mwanamke kuwa mali ya mwanamume. Mwanamke yuko chini ya mwanamume katika jamii,kulingana na kanuni zenyewe.

Wakene (*Natala,* 1997) anaona kuwa yeye ndiye mdhibiti wa mali baada ya nduguye Tango Mwina kuaga dunia. Kwa hivyo, Natala anapokataa kurithiwa, anaagizwa atafute pa kuhamia. Kuhusu watoto, Wakene anaona ni wa familia ya Tango Mwina. Wakene mwenyewe anapanga kuliuza shamba ili atumie katika kampeni za kisiasa. Newland (1997:167) anaeleza kuwa hali ambapo mwanamke anatengwa katika masuala ya urithi. Anabainisha jamiii katika nchi nyingi ambapo mwanamke hawezi kurithi ardhi. Anasema ardhi hurithishwa kutoka baba hadi mwanawe wa kiume au mwanamume yeyote wa ukoo. Hali hii anavyodai Newland, husababisha utegemezi mkubwa miongoni mwa wanawake. Natala anaonekana kuelewa hali itakayomfika akirithiwa. Anamwambia Mama Lime, *Na nafasi yangu nyumbani ndogo* (uk.39). Anafahamu kuwa kuriyhiwa huko kutamnyima uhuru wake. Kwa hivyo, anakataa kurithiwa na Wakene.

### 4.4 Ukosefu wa Ushirikiano Miongoni mwa Wanawake Wenyewe.

Ushirikiano ni msingi wa ufanisi katika shughuli yoyote. Bila ushirikiano, ufanisi hauwezi kupatikana au hupatikana kwa shida. Wahenga walisema kuwa umoja ni nguvu

utengano ni udhaifu. Akiangazia nafasi ya mwanamake, Nyamberi (1997:52) anadai kuwa kikwazo kinachozikabili harakati za kumkomboa mwanamke ni ukosefu wa ushirikiano miongoni mwao. Anasema kuwa wanawake wenyewe wanashughulikia masuala ya kibinafsi. Anasema kuwa kila mmoja anashughulikia mahitaji ya kibinafsi na hivyo, kudidimiza juhudi za mapambano yenyewe.

Naye Maxine katika makala aliyochangia katika ripoti ya *The Future Education In Eastern Africa* (1997:83) anatoa tathmini yake. Ana maoni sawa na ya Nyamberi. Kwa hivyo, anapendekeza ushirikiano miongoni mwa wanawake wenyewe. Hatua hii kwa maoni yake, itawasaidia kujiinua kijamii na pia kiuchumi. Anatoa mfano wan nchi ya Uganda ambayo imetenga nyadhifa fulani za uongozi hususan kwa wanawake. Lengo lenyewe lilikuwa ni kuhimiza demokrasia na kuwainua wanawake kihadhi. Maxine anawahimiza wanawake washirikiane badala ya kulumbana wao kwa wao.

Katika *Natala* (1997), Natala amelazimika kumeza machungu kwani wanaume kwa wanawake wanambagua. Katika harakati zake za kujitetea, Mama Lime anashirikiana na Wakene kumwadhibu. Mama Lime mwenyewe anamchochea Wakene atoe 'Karatasi yenyewe' chumbani. Huu ni wakati Natala alipotoka kuwashughulikia wanawe (uk. 53). Bala na Gane wanapojitokeza kumsaidia, Mama Lime mwenyewe anawatahadharisha dhidi ya kuingilia mambo ya wenyewe. Awali, Tila alikuwa amemjia kwa fujo na kumkumbusha kuwa hapo ni kwa Tango Mwina (mali ya mumewe) wala si kwa yeye Natala. Tila anasema, *Ukikasirika utafanya nini? Niko kwa kaka ya mume wangu!* (uk. 5). Tila na Mama Lime wangeshirikiana na Natala, wangefanikisha harakati zake Natala

kuimarisha hali ya mwanamke. Lakini wao ndio vikwazo katika mapambano yenyewe. Hali hii imedhihirishwa na Penina Muhando katika *Nguzo Mama* (1982). Anamtumia Bi. Nane kuonyesha juhudi za mapambano dhidi ya hali dhaifu ya mwanamke katika jamii. Lakini anakabiliwa na pingamizi ya wanawake kama Bi. Nne. Wanawake wanakosa ushirikiano unaohitajika kuinua hali zao kijamii. Kutokana na ukosefu huu wa ushirikiano, Nguzo Mama inakosa kuinuliwa. Hii ni taashira ya kukosa kuinuka hali ya mwanamke (mama) katika jamii kwa kukosekana ushirikiano.

**Hitimisho**

Katika sura hii, tumezifafanua baadhi ya changamoto zinazoonekana kukwamiza ufanisi katika kujenga usawa wa kijinsia katika *Natala* na *Kifo Kisimani*. Tumeziainisha changamoto zenyewe katika makundi manne huku tukidondoa mifano mwafaka.

Kwanza tumeangazia asasi za kitamaduni zinazoonekana kudidimiza mwanamke katika dhulma. Mwanamke amepewa nafasi duni katika jamii. Mwanamume naye amepewa udhibiti wa mila na desturi zinazomgandamiza mwanamke.

Pili, tumeangazia hali ya kutojua miongoni mwa wanawake. Imebainika kuwa wanawake wengi wamebakia katika hali dhaifu kwa sababu ya kutoelewa na kutambua haki zao. Na kwa sababu ya hali hii, wanakosa kupigania haki zenyewe. Kuna haki fulani wanazofaa kufurahia lakini wananyimwa kwa sababu ya kutojua kwao.

Tatu, tumedhihirisha masuala ya kiuchumi yanayompa udhibiti wa kiuchumi wa mwanamume na kumtenga mwanamke. Kwamba, mifumo ya kiuchumi humpendelea na kuzidi kumwinua mwanamume. Lakini mwanamke anaendelea kuwa mtegemezi wa mwanamume. Haya yanaonekana kurutubishwa na utamaduni, kasumba za kikoloni na mfumo wa kijamii kwa ujumla.

Hatimaye, tumeangazia ukosefu wa ushirikiano ambao unabainika miongoni mwa wanawake wenyewe. Wanawake aghalabu wanalumbana wao kwa wao badala ya kushirikiana kukabili dhuluma zinazowakabili katika jamii inayomwenzi mwanamume.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala* (1997) na *Kifo Kisimani* (2001). Kwa kuongozwa na nadharia ya Ufeministi, tulijikita katika tapo la eneo la Afrika. Hii ni kwa sababu tamthilia zenyewe zimetungwa katika mandhari ya Kiafrika. Kwa hivyo, tumeteua tapo lenyewe kimuktadha.

### 5.1 Muhtasari wa Matokeo ya utafiti.

Nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani* ni mambo yanayojitokeza wazi . Mwandishi amefaulu kudhihirisha nafasi anayopewa mwanamke katika jamii ya ki-ubabedume. Ameonyesha namna jamii ya aina hii inavyomchukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu,anayepewa nafasi chukivu. Pia,amechangia kwa kumwinua mwanamke kihadhi kwa usawiri chanya.

Katika utafiti wenyewe tulikuwa na madhumuni mawili. Kwanza, tulilenga kuchunguza nafasi anayopewa mwanamke katika jamii. Tuliangazia nafasi yenyewe kwa kurejelea jinsi inavyodhihirika katika tamthilia hizi. Pili, tulichunguza changamoto zinazokabili ufanisi wa harakati zenyewe kama zinavyodhihriishwa na mwandishi katika tamthilia zake. Kutokana na utafiti wetu, tuliainisha nafasi ya mwanamke kuwili: Nafasi chukivu/hasi na nafasi chanya. Matokeo yetu yamedhihirisha kuwa, mwanamke anadhalilishwa na kudunishwa katika jamii inayomkweza na kumwenzi mwanamume. Jamii yenyewe humdhalilisha na kumdunisha mwanamke kwa namna tofauti. Matokeo

yenyewe ni kama yafuatayo; mwanamke anachukuliwa kuwa chombo cha kumfurahisha mwanamume kwa kuntumbuiza na hata kuzima ashiki zake za kiume. Mwanamume hulelewa kwa kumwanda kuwa mbabe na mwanamke kuwa mtumishi wake. Kithaka wa Mberia amefaulu kusawiri hali hii kwa kutumia wahusika wanawake kama Nawira na Natala, Wanaume kama Wakene (*Natala)* na mhudumu wa Jengo la Ufuo wanaomchukulia mwanamke kuwa mtumbuizaji wa mwanamume. Kwao, hiyo ndiyo nafasi ya kiumbe huyu duni.

Jamii nyingi za ki-ubabedume humtenga mwanamke kiuchumi kama tulivyobainisha katika sura za awali, mwanamke mwenyewe hana kibali scha kumiliki au kurithi mali katika jamii. Huu ni udhalishaji dhidi ya mwanamke. Na Kithaka wa Mberia amefaulu kuangazia suala hili kupitia mhusika mkuu Natala katika *Natala.* Jamii hii inampa mwanamume udhibiti na umiliki wa nyenzo za uzalishaji mwanamume. Mwandishi huyu ametuchorea picha halisi inayojitokeza katika jamii. Hii ni picha inayoangazia hali ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika. Kwa hivyo, mwandishi amefaulu pakubwa.

Kwa sababu ya kutomiliki chochote, mwanamke anakosa kupiga hatua kiuchumi. Matokeo yake ni yeye kuwa mtegemezi wa mwanamume kiuchumi. Kwa sababu hiyo, mwanamke hulazimika kunyenyekea mbele ya mwanamume na kuitikia matakwa ya mwanamume. Ni wanawake wachache pekee (kama Natala) wanaojasiria kupinga nafasi ndogo wanayopewa nyumbani. Mwandishi huyu amebainisha hali hiyo. Miongoni mwa wahusika wengi waliosawiriwa katika *Natala*, ni Natala pekee anayejasiria kupinga hali

hii. Anapopendekezewa kurithiwa, anapinga na kuamua kupitia 'njia nyingine' kwa sababu hataki kupewa nafasi ndogo jamii.

Jamii ya ki-ubabedume humchukulia mwanamke kuwa mtu mwovu. Humnasibisha na maovu ya kijamii kama ukahaba, umbeya, ugomvi, ubarakala na hasira nyingi. Kwa kusawiriwa hivyo, mwanamke huonekana kuwa mtu asiyefaa kushikilia wadhifa wowote. Badala yake anafaa kuongozwa, kuelekezwa na kufanyiwa maamuzi. Kithaka wa Mberia ameangazia suala hili katika *Natala* na *Kifo Kisimani*. Nyadhifa zote za uongozi zinashikiliwa na wanaume, na maamuzi pia aghalabu yanafanywa na wanaume. Kwa hivyo, amedhihirisha hali yenyewe jinsi ilivyo katika jamii zinazotawaliwa na mfumo wa ki-ubabe-dume. Mfumo wenyewe huwa na utawala unaosimamiwa na kamati ya wazee (wanaume). Mashauri, maamuzi na hukumu hufanywa na baraza lenyewe.

Kwa kuangazia hali hizi, mwandishi ameonekana kuelewa udhalilishaji, udumishwaji na nafasi chukivu wanayopewa wanawake katika jamii. Kwa maoni yetu, mwandishi huyu amefaulu kubainisha nafasi chukivu anayopewa mwanamke katika jamii hizi.

Licha ya hayo, Kithaka wa Mberia amefaulu kumwinua na kumjenga mwanamke kihadhi. Kupitia tamthilia zenyewe, amefaulu kumtambulisha mwanamke na mchango wake muhimu katika jamii. Anaizindua jamii ili iweze kutambua umuhimu huu na kuutilia maanani katika kujenga jamii. Mwandishi mwenyewe ameangazia bidii za mwanamke. Anatumia wanawake kama Tanya, Natala, Atega kudhihirisha bidii za wanawake. Kutokana na bidii zao, wanawake wenyewe wanafanikisha shughuli zao

kijamii: kazi za nyumbani na malezi (walizowajibishwa na jamii). Bidii zenyewe zinawawezesha pia kushirikiana na wazalendo wengine kupigana ukombozi wa jamii (*Kifo Kisimani*, 2001).

Mwandishi huyu pia ameibua suala la ushauri. Anamtambua mwanamke kuwa mtu anayeweza kushauri, kuzindua na hata kuwatahadharisha wanajamii. Kwamba uelewa wa mwanamke na akili yake tambuzi ni muhimu. Humweka katika nafasi nzuri ya kushauri, kuzindua na kutahadharisha dhidi ya maovu ya kijamii. Kwa kuwatumia wahusika Tanya, Nyalwe na Atega, mwandishi amefaulu kuangazia nafasi hii.

Uchunguzi wetu pia umebainisha kuwa mwanamke ni mtu jasiri. Mwandishi amefaulu kumwomba mwanamke jasiri anayeweza kukabiliana na changamoto na hali ngumu. Mwandishi amefaulu kubainisha nafasi hii. Wanaume wenyewe wanakumbana na hali za kutamausha lakini wanajikakamua kuzishinda changamoto zinazowakabili. Kwa hivyo, mwandishi anaelekea kuizindua jamii kutambua sifa kama hizi miongoni mwa wanawake na kuzijenga.

Katika madhumumi yetu ya pili, tulilenga kuchunguza changamoto zinazokwaza harakati za kumkomboa mwanamke. Kama inavyobainika, mwandishi anaonekana kutambulisha baadhi ya changamoto zinazokabili harakati hizi. Mojawapo ikiwa ni asasi za kitamaduni. Asasi zenyewe zinamkandamiza mwanamke na kumpa nafasi duni katika jamii, na wakati huo huo kumpendelea mwanamume. Pili, kuna hali ya kutojua miongoni mwa wanawake. Wanawake wenyewe aghalabu hawajui haki zao, hivyo hukosa kuzipinga

kwa sababu ya kutojua. Ni wachache wanaozijua haki zenyewe. Tatu, ni masuala ya kiuchumi yanayoonekana kumkandamiza mwanamke. Mwanamume aghalabu hupiga hatua kiuchumi lakini mwanamke amezidi kubakia pale pale kiuchumi. Hatimaye kuna hali ya utengano miongoni mwa wanawake Wanawake wenyewe wangetarajiwa kusaidiana katika kuhimizana, kuinuana na kuzinduana. Lakini, yanayotokea aghalabu ni tofauti. Wanawake wengi hulumbana na kuchimana. Mwandishi ameweza kubainisha changamoto zenyewe vilivyo. Amefanya hivyo ili kutoa mchango wake wa kuwazindua wanajamii kuchukua hatua ifaayo kujenga jamii. Amebainisha mchango muhimu wa mwanamke katika jamii. Utafiti wetu umefaulu katika kutathmini mchango wa msanii katika kuangazia nafasi anayopewa mwanamke katika jamii. Mihimili ya nadharia ya Ufemenisti ni kuangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakumba wanawake katika jamii ya ki-ubabe-dume. Mwandishi mwenyewe ameangazia na hivyo,kuitafakarisha jamii na hasa wanawake.

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Ufemenisti wa Kiafrika,unaotambua utamaduni kuwa suala kuu. Mwandishi amedhihirisha uelewa wake kuhusu nafasi chukivu anayopewa mwanamke katika jamii. Nafasi yenyewe inarutubishwa na utamaduni unaodhibitiwa na mfumo wa kiume. Pia, ametoa mchango wake muhimu katika harakati za kumkomboa mwanamke. Ameonyesha nguvu na mchango muhimu wa mwanamke katika ujengaji wa jamii upya. Katika tamthilia hizi, ameonyesha nguvu za mwanamke kupitia Natala (*Natala*,1997),Tanya, Atega, Nyalwe, Andua na Azena (*Kifo Kisimani*,(2001).

Utafiti wetu hivyo basi, umefaulu kutathmini mchango wa mwandishi katika ukombozi wa mwanamke katika jamii ya ki-ubabe-dume. Pia, amefaulu kudhihirisha changamoto zinazokabili harakati hizi. Kupitia tamthilia zenyewe,,ameweka wazi changamoto zenyewe.

**Mapendekezo kwa Tafiti za baadaye**

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya Ufeministi. Katika nadharia yenyewe, tumejikita katika tapo la eneo la Afrika. Kwa hivyo, tunapendekeza tafiti za baadaye ziweze kuangazia mada yenyewe kwa kujikita katika tapo jingine la Ufeminsiti. Hii ni kwa sababu tafiti zenyewe zinanuiwa kuimarisha jamii kwa ujumla. Kila tapo, kwa hivyo itachangia katika kuleta suluhu kwa matatizo yanayotukabili katika jamii. Na kila tapo lina mchango wake. Utafiti pia unaweza kufanywa kwa kuongozwa na nadharia nyingine kama Umarx. Hii ni kwa sababu kuna baadhi ya wataalamu wanaochukulia suala la jinsia kama aina mojawapo wa utabaka katika jamii. Mtafiti pia anaweza kuangazia mchango wa asasi za kitamaduni katika udidimizaji wa harakati za ukombozi wa wanawake. Tumeangazia kama changamoto lakini zinaweza kuziangazia kama mada kamili katika utafiti.

## MAREJELEO


Abidi, S.A. (1997) *The Future Education in Eastern Africa*. *Proceeding of the 2nd PWPA East African Regional Confernece, Kampala*. Professors World Peace Academy.

Akua, K (2003) (Mh*) Women and the Law In West Africa*. Accra: Women and the Law in West African Human Rights Centre.

Arnfred, S (2004) (Mh) *Re-thining Sexual;ity In Africa*. Almgrist & Wicksell Tryskers AB

Beauvoir, Simone de (1949) *The Second Sex*. London: Dana Campbell Publishers.

Georgina, A (1995) (Mh) *A Diplomacy of the Oppressed: New Direction in International Feminism*.

Greer, G (1980) *The Female Eunuch*. London: Crafton Books.

Imbuga, F. (1976) *Betrayal In The City*. Nairobi:East Africa Education Publishers.

Katola, E (2006) "Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike" TAsnifu ya M.A Chio Kikuu cha Nairobi, Haijachapiswa.

Kisiroche, I.R. (2008) "Sauti ya Mwanamke Dhidi ya Ubabe-dume katika Tamthilia za Kiswahili." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Maringi, H (2007) "Upembezwaji wa mwanamke katika *Utenzi wa Fatumah*" Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapiswa.

Mazrui, A (1982) *Kilio cha Haki*: Nairobi: Longman Kenya.

Mberia, K (1997) *Natala*. Nairobi: Marimba Publications.

________(2001) *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publishers

Millet, K (1969) *Sexual Politics*. New York: Doubleday and Company Ic.

Miriam Ba (1981) *So Long A Letter.* London: Heinamann.

Mirikau, S. (2011) “Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Wamitila” Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mogambi, K (1983) “Hali ya Wanyonge kama inavyojitokeza katika Riwaya za S. Mohamed”. Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mohamed, S.A (1980) *Utengano.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mugambi, E (1982) “Uhakiki wa Maudhui Katika Tamthilia za Kikenya zilizochapishwa.” Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi.

Muhando, P (1982) *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mukobwa, M (1985) “Maendeleo ya Kimaudhui katika Tamthilia Tano za Ebrahim Hussein”. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Moi, T (2002) *Sexual/Textual Politics: Feminism Literary Theory.* London: Routledge.

Mulila, J. (2009) ‘`Usawiri chanya wa Wahusika Wanawake Katika Tamthilia za *Zilizala* na *Chamchela’’* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mutua, J.M. (2007) “Mitazamo ya Vijana na Wazee kuhusu Ukombozi wa Wanawake”. Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Newland, K (1979) *The Sisterhood of Men: The Impacts of Women’s changing roles on social and economic life around the world*. New York: W.W Norton.

Ndungo, C (1985) “Wanawake na Mabadiliko katika Fasihi ya Kiswahili” Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Njogu, K na Chimerah R.(1999) *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nunes, M na Dearna, W (1972) *The Lace Ghetto*. Toronto West: New Press.

Nyamberi, H (1997) "Mwamko wa Mwanamke katika Tamthilia Nne za Penina Muhando" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.

Onyoni,J (2012) ''Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Tamthilia za *Natala* na *Mama Ee.''* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Pilcher, J na Imelda, W (2004) *50 Key Concepts in Gender Studies*. Los Angeles: Sage Publication.

Silvard, R (1985) Women*….a World Survey*. Washington DC: World Priorities.

Steady, F.C (1981) *The Black Women Cross-Culturally*. Cambridge: Schenkam publishing co. inc.

Taylor, D (1985) *Women*: *A World Report*. Oxford: New International Cooperative.

Tuckewell, S na Moore, K (1975) *We Women: A dossier on Women Development*. Cambura: Australian Council of Overseas Aid.

UN (1995) The *Worlds's Women (2000). Trends and Statistics*. New York: United Nations.

Wafula, R na Kimani, N (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Wamitila, K (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix

___________ (2004) (Mh) *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Focus Books.

Wanjiku, K na Akinyi, N (1993) *Celebrating Women's resistance. A case study of Women Groups Movement in Kenya*. Nairobi: Africa Women Perspective.

Wollstonecraft, M (1792) A *Vindication of Rights of Women*. Boston: Peter Edes